# WAKAA, UWASILISHAJI USEMI NA WAHUSIKA KATIKA HOTUBA TEULE ZA WANASIASA WA KENYA


**MUKONAMBI KEKONEN STANLEY**

**C50/CE/20699/2022**


**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi wasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutunukiwa shahada yoyote.

Sahihi:................................ Tarehe: 10/11/2025


**Mukonambi Kekonen Stanley**

**C50/CE/20699/2022**


Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi wa Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:................................ Tarehe: 10/11/2025


**Dkt. Titus Kaui**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**



KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES
10 NOV 2025
NAIROBI
KENYATTA UNIVERSITY

## TABARUKU

Kwa mama mpenzi Mary Muthoni Kibe. Upendo wako, maombi yako kwa Maulana kunihusu, nguvu zako, na msaada wako usiotetereka ulifanya hili kuwezekana.

## SHUKRANI

Ninatoa shukrani za dhati kwa Mola kwa neema na nguvu zilizoniongoza katika safari hii ya masomo. Tangu nilipong'oa nanga katika safari hii, alinijalia afya njema, akanipa uzima wa kimwili na kiakili na kugharamia mahitaji yote hadi sasa nafikia ukingo wa hatua hii ambao naamini anautumia kuufungua mlango mwingine. Sifa na utukufu ni zako Mungu!

Shukrani za dhati kwa msimamizi wangu Dkt. Titus Kaui kwa ushauri, mawaidha na mwongozo wake. Asante kwa kunivumilia, kuwa tayari kunielekeza na kwa kutenga muda kupitia kila neno katika tasnifu hii licha ya kubanwa na majukumu mengi mengine. Mungu akuneemeshee afya bora na azidi kukunyunyizia baraka zake. Sitawasahau Mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili Prof. P. Githinji. Wewe kwangu si mshauri mwema pekee bali pia mlezi mwema. Kila mara ungeacha shughuli zako pale afisini kutushauri na kutueleza kuhusu mazuri yanayotungoja baadaye tukiendelea kupanda daraja hili la masomo. Aidha, Prof. R. Wafula, sitawahi isahau ile simu uliyonipigia ukiniulizia kuhusu nilipofika katika mchakato huu na kunipa motisha ya kujibidiisha.

Ninawashukuru wahadhiri wangu waliojitolea kutufunza kozi mbalimbali zilizoweka msingi wa kazi hii. Wahadhiri hawa ni Prof. R. Wafula, Prof. P. Ngugi, Prof. L. Chacha, Dkt. Masinde, Dkt. Arege, Dkt. Ngugi, Dkt. Mutugu, Dkt. Onyango, Dkt. Osore na Dkt. J. Murithi, aah nani kama wewe? Mmeninoa na kunipa makali ya maarifa sio tu katika taaluma ya Kiswahili bali pia katika mambo ya kimaisha. Mungu awabariki.

Kwa upendo, namshukuru mama Mary Muthoni Kibe. Maombi yako ya kila mara kwake Mungu uliyoniombea kwa kweli yamejibiwa. Maswali yako kuhusu nilipofika na siku ya kufuzu kila mara yalinifaa na kuniwezesha kujikaza mhanga. Asante kwa

ndugu zangu Margaret Wambui, John Nakitare na Jemimah Nafula kwa kunivumilia na kunitakia mema. Baraka zake Mungu ziwe nanyi msije mkapungukiwa.

Shukrani kocho kocho kwa Nasambu Chamao vilevile. Niseme lipi, niache lipi? Haya yalifanya nikakupata.

Hatimaye, nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana kila mara katika kozi hii ambao ni Nicodemus Muneeni, Edith Nyokabi, Kimindu Mwongeli, Faith Matanga na Kerongo Brenda. Siwezi kuwasaza Stephen Mwendwa, wewe si mwandani tu bali ndugu, na Wilson Oluchili. Nawatakia mema katika maisha yenu.

Kwa wote wengine ambao walinisaidia kwa njia moja au nyingine kufikia kiwango hiki. El Makadara awafae daima dawamu!

## YALIYOMO

**UNGAMO** ........................................ ii
**TABARUKU** ........................................ iii
**SHUKRANI** ........................................ iv
**YALIYOMO** ........................................ vi
**ORODHA YA AKRONIMU** ........................................ x
**MAELEZO YA DHANA NA ISTILAHI MUHIMU** ........................................ xi
**IKISIRI** ........................................ xii
**ABSTRACT** ........................................ xiii
**SURA YA KWANZA** ........................................ 1
**UTANGULIZI** ........................................ 1
1.0 Usuli wa Mada ........................................ 1
1.1 Suala la Utafiti ........................................ 3
1.2 Malengo ya Utafiti ........................................ 3
1.3 Maswali ya Utafiti ........................................ 4
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................ 4
1.5 Upeo na Mipaka ........................................ 5
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................ 6
1.6.1 Tafiti Zinazohusu Usimulizi ........................................ 6
1.6.2 Tafiti Zinazohusu Hotuba ........................................ 8
1.7 Msingi wa Nadharia ........................................ 9
1.8 Mbinu za Utafiti ........................................ 11
1.8.1 Muundo wa Utafiti ........................................ 12
1.8.2 Mahali pa Utafiti ........................................ 12
1.8.3 Sampuli na Usampulishaji ........................................ 12
1.8.4 Ukusanyaji Data ........................................ 13
1.8.5 Uchanganuzi wa Data ........................................ 13
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ........................................ 14
1.9 Maadili ya Utafiti ........................................ 14
**SURA YA PILI** ........................................ 15
**WAKAA KATIKA HOTUBA TEULE ZA WANASIASA** ........................................ 15
2.0 Utangulizi ........................................ 15
2.1 Mpangilio ........................................ 16
2.1.1 Analepsia ........................................ 16

2.1.1.1 Analepsia Tawasifu ....... 17
2.1.1.2 Analepsia Wasifu ....... 19
2.1.1.3 Analepsia ya Nje ....... 21
2.1.1.4 Analepsia ya Ndani ....... 22
2.1.1.5 Analepsia Mseto ....... 22
2.1.2 Prolepsia ....... 23
2.1.2.1 Prolepsia ya Nje ....... 24
2.1.2.2 Prolepsia ya Ndani ....... 26
2.1.2.3 Prolepsia Wasifu ....... 26
2.1.2.4 Prolepsia Tawasifu ....... 27
2.2 Muda ....... 28
2.2.1 Udondoshi ....... 29
2.2.1.1 Udondoshi Bayana ....... 29
2.2.1.2 Udondoshi Usio Wazi ....... 30
2.2.1.3 Udondoshi Batini ....... 31
2.2.1.4 Udondoshi Dhahiri ....... 31
2.2.2 Mtuo ....... 32
2.2.3 Muhtasari ....... 33
2.2.4 Onyesho ....... 34
2.3 Umara/ Idadi Marudio ....... 35
2.3.1 Usimulizi Mosi ....... 36
2.3.2 Usimulizi Rudufu ....... 36
2.3.3 Usimulizi Banifu ....... 38
2.4 Hitimisho ....... 38
**SURA YA TATU ....... 40**
**USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA HOTUBA TEULE ....... 40**
3.0 Utangulizi ....... 40
3.1 Wahusika ....... 40
3.2 Usawiri wa Wahusika ....... 41
3.3 Mbinu za Kuwasawiri Wahusika ....... 42
3.3.1 Usawiri wa Moja kwa moja/ Bainishi ....... 42
3.3.2 Usawiri Usio wa Moja kwa Moja (Usawiri Timbe) ....... 46
3.3.2.1 Mazingira ....... 47
3.3.2.2 Usemi ....... 49

3.3.2.2.1 Jinsi anavyozungumza mhusika ........................................ 50
3.3.2.2.2 Mazungumzo Kujihusu au Kuwahusu Wahusika Wengine ........... 51
3.3.2.2.2.1 Mhusika na Wasifu wake ........................................ 51
3.3.2.2.2.2 Mhusika na Wasifu wa Mhusika Mwingine ........................ 53
3.3.2.3 Muonekano wa Nje ........................................ 53
3.3.2.4 Analojia ........................................ 54
3.3.2.4.1 Majazi ........................................ 54
3.3.2.4.2 Ulinganuzi wa Wahusika ........................................ 56
3.3.2.5 Matendo ........................................ 56
3.3.2.5.1 Tendo la Utekelezaji ........................................ 57
3.3.2.5.1 Tendo la Kunuia ........................................ 57
3.4 Hitimisho ........................................ 57
**SURA YA NNE ........................................ 58**
**UWASILISHAJI USEMI DHIMA ZAKE, ZA WAKAA NA WAHUSIKA .......... 58**
4.0 Utangulizi ........................................ 58
4.1 Uwasilishaji Usemi ........................................ 58
4.1.1 Usemi Halisi ........................................ 59
4.1.2 Usemi Taarifa ........................................ 61
4.1.3 Usemi Halisi Huru ........................................ 64
4.1.4 Usemi Taarifa Huru ........................................ 65
4.2 Dhima za Vipengele vya Wakaa, Wahusika na Uwasilishaji Usemi katika Hotuba Teule za Wanasiasa wa Kenya ........................................ 66
4.2.1 Kujenga Maudhui ........................................ 66
4.2.1.1 Kuendeleza siasa ........................................ 68
4.2.1.2 Kukashifu ufisadi ........................................ 70
4.2.1.3 Kukuza uchumi ........................................ 71
4.2.1.4 Kuendeleza Uwiano na Utangamano wa Kitaifa ........................................ 73
4.2.2 Kuchimuza Fani au Tamathali za Usemi ........................................ 74
4.2.2.1 Majazi ........................................ 75
4.2.2.2 Sitiari ........................................ 76
4.3 Hitimisho ........................................ 78
**SURA YA TANO ........................................ 79**
**MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........................................ 79**
5.0 Utangulizi ........................................ 79

5.1 Muhtasari wa Utafiti........................................................................................79
5.2 Matokeo ya Utafiti ..........................................................................................81
5.3 Mchango wa Utafiti.........................................................................................83
5.4 Matatizo yaliyoukabili Utafiti ........................................................................83
5.5 Mapendekezo ...................................................................................................84
5.6 Hitimisho..........................................................................................................85
**MAREJELEO ......................................................................................................86**
**Kiambatisho A: Tovuti za hotuba.......................................................................90**
**Kiambatisho B: Kibali cha utafiti .......................................................................91**

## ORODHA YA AKRONIMU

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili la Zanzibar |
| BBI | Building Bridges Initiative |
| Bw. | Bwana |
| Dkt. | Daktari |
| JP | Jubilee Party |
| KICC | Kenyatta International Convention Centre |
| MCA | Member of County Assembly |
| Mhes. | Mheshimiwa |
| NASA | National Super Alliance |
| NCIC | National Cohesion and Integration Comission |
| NKJV | New King James Version |
| ODM | Orange Democratic Movement |
| PNU | Party of National Unity |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| TNA | The National Alliance |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UDA | United Democratic Movement |
| URP | United Republican Party |

## MAELEZO YA DHANA NA ISTILAHI MUHIMU

**Dhamira:** Dhana hii inarejelea kiini cha jambo au habari iliyosimuliwa ama kuandikwa.

**Hadithi :** Hii ni habari kuhusu mambo yaliyofanyika/ kutendeka.

**Hotuba:** Haya ni maelezo maalum yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya hadhira.

**Naratolojia:** Hii ni nadharia inayojishughulisha na uchanganuzi wa muundo wa masimulizi.

**Siasa:** Huu ni mfumo unaotumika katika kuendeleza shughuli za kijamii katika nchi. Huhusisha masuala k.v utamaduni, Uchumi wa taifa na mfumo wa uongozi. Aidha huhusu mitazamo tofauti ya kidini, kabila na thamani ambayo husababisha migogoro katika jamii na hunuia kutatua migogoro hio.

**Usimulizi:** Ni mchakato wa mawasiliano ambapo masimulizi au hadithi kama ujumbe hupitishwa na msemaji hadi kwa msemewa au hadhira.

**Wakaa:** Kipengele kinachoonyesha uhusiano wa kiufuatano kati ya hadithi na matini, yaani muda unaotumika katika kuendeleza matukio katika kazi ya fasihi.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Baadhi ya wanasiasa hutumia hotuba zinazovuta makini ya wasikilizaji na wafuasi wao kwa mitindo tofauti. Mojawapo ya mbinu hizi za kimtindo ni usimulizi. Utafiti huu ulichunguza vipengele vya usimulizi; wakaa, uwasilishaji wa usemi na wahusika. Wakaa ni mpangilio wa matukio katika hadithi. Uwasilishaji wa usemi ni namna ambavyo maana hutolewa kwa kutumia lugha ilhali wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaoendeleza kazi ya kifasihi. Malengo ya utafiti huu ni: kubainisha vipengee vya wakaa, uwasilishaji wa usemi na wahusika katika hotuba teule na kujadili dhima ya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule. Nadharia iliyotumika ni ya Naratolojia kwa kuzingatia mawazo yake Rimmon-Kenan. Mtazamo wake ni wazi kwani huwasaidia wasomaji kutofautisha kwa urahisi viwango vya masimulizi na kuchanganua matini kwa hatua. Aidha, haujatumika na tafiti nyingi ikilinganishwa na ule wa Gerald Genette. Mihimili yake ilifaa kwani iliweka wazi vipengele ambavyo vilishughulikiwa na kutathmini nafasi yavyo katika uelewekaji wa hotuba teule. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulitumika kuteua hotuba teule za Rais mstaafu Uhuru Kenyatta wa chama cha TNA na JP, Mhes. Raila Odinga wa chama cha ODM na Rais Dkt. William Ruto wa chama cha URP, JP na UDA zilizotolewa kati ya mwaka 2013 hadi 2023. Utafiti ulifanyika maktabani ambako data ilikusanywa kwa njia za usomaji makini kwa kupitia makala, nyaraka, majarida, tasnifu za awali na kutazama na kusikiza makala ya mtandao wa *YouTube.* Ufafanuzi wa kimaelezo kwa kuzingatia nadharia ulitumiwa kutolea matokeo ya utafiti ambayo yamewasilishwa kwenye vijimada vilivyomo katika sura tano za tasnifu hii. Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango katika taaluma ya fasihi kwa wahakiki na wanafunzi kufahamu nafasi ya vipengee hivi katika hotuba. Aidha, unawafaidi wahakiki na watafiti wa fasihi kwa kuwaelekeza jinsi ya kuhakiki hotuba.

## ABSTRACT

This study examined the narrative time, speech delivery and characters in selected speeches of Kenyan politicians. Some politicians use speeches that attract their listeners by using various stylistic methods. One of these stylistic techniques used is narration. This work focuses on the elements of narrative – narrative time, speech delivery and characters. Narrative time is the order of events in a story. The presentation of speech is the way in which meaning is given using language, while the characters are artistic creatures who develop the literary work. The objectives of this research are: to determine the elements of narrative time, presentation of speech and characters in selected speeches of selected politicians and discuss the role of narrative time, presentation of speech and characters in selected speeches. The Rimmon-Kenan perspective in Narratology theory guided the research. His ideas provide a clear systematic framework that helps readers easily distinguish between narrative levels for text analysis. Also, they've not been applied in many research work compared to the ideas of Gerald Genette. Its tenets are appropriate as they set out the elements that were addressed and evaluated their place in the understanding of the selected speech. Purposive sampling techniques was used to select speeches by former president Uhuru Kenyatta, Hon. Raila Odinga and Hon. William Ruto given between the years 2013 and 2023. The research was conducted in the library where data was collected through careful reading through articles, documents, journals, related theses and watching and listening to videos on *YouTube.* Descriptive interpretation based on the theory was used to present the results of the study that have been presented in subtitles of the five chapters in this thesis. The results of this study will contribute to the literary profession for critics and students of literature to understand the role of these elements in speech. In addition, it will benefit literary critics and researchers by instructing them on how to review and analyze a speech.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Mulokozi (1996) alitafiti na kuainisha fasihi simulizi ya Waswahili katika kumbo sita mahususi kwa ajili ya kufundishia. Hizi ni semi, mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi simulizi na ngomezi. Aliainisha hotuba chini ya utanzu wa mazungumzo. Kwa upande mwingine, Kamusi ya TUKI (2019) inaeleza usimulizi kama utambaji au maelezo ya jambo fulani katika hadithi. Nayo simulizi ni maelezo ya tukio fulani au fasihi inayotolewa na kupokezanwa kwa kusimuliwa.

Barry (1995) anasema kuwa usimulizi ni mtaala wa jinsi simulizi huleta maana. Naye Wamitila (2008) anaonyesha vipengee muhimu katika usimulizi na kuviainsha kama wakaa, uwasilishaji wa usemi na wakala wa usimulizi. Wakaa ni uhusiano wa kiufuatano wa matukio kati ya hadithi na matini (Rimmon-Kenan 1983). Kipengele hiki cha usimulizi huonyesha kuwa wahusika huishi, matukio kufanyika ambayo ni kiini cha maudhui. Hivyo, utafiti huu ulichunguza jinsi wanasiasa hupanga matukio katika hotuba zao, muda unaochukuliwa na tukio na ni mara ngapi tukio hilo hurejelewa na wanasiasa.

Genette (1972) anasema kuwa uwasilishaji usemi unatokana na kitendo cha kuongea. Kauli yake inaweza kufasiriwa kumaanisha kuwa bila usimulizi hakuna kauli. Huu ndio msingi wa utafiti kwani hotuba ni kauli. Hadithi huwasilishwa katika usemi halisi na usemi taarifa (Kwaka, 2018). Prince (1982) anapigia haya upato kwa kuendeleza kuainisha usemi katika usemi halisi, usemi halisi huru, usemi taarifa na usemi taarifa huru.

Kasper na Wuckel (2015) wanasema mhusika ni picha ambayo huchorwa na fasihi na huwa kiini cha vitu vyote vipya. Mawazo yao yanasawiana na yale ya Njogu na Chimerah (1999) wanaposema kuwa mhusika ni kiumbe apatikanaye katika kazi za fasihi na anafanana na binadamu kwa kiasi fulani.

Rimmon-Kenan (keshatajwa) anawachunguza wahusika kama miundo katika simulizi, anasisitiza maumbile yao tofauti kwa kupendekeza kuwa hawafafanuliwi tu kwa sifa zao bali ni zao la mbinu za masimulizi.

Kwa hivyo, wahusika huhitajika kuwepo ili kutenda matukio katika hadithi. Wao ndio nguzo kuu katika kubeba maudhui na dhamira ya mtunzi (Wamitila, 2008). Utafiti huu ulichunguza na kuonyesha jinsi wanasiasa hutumia ujuzi katika hotuba kuwasuta wapinzani wao kutegemea ujumbe wanaonuia kuwafikishia wanajamii. Ulichunguza jinsi wanavyowaumba kwa kurejelea sifa zao mbali mbali na mbinu ya kuwawasilisha kwa hadhira yao.

Mwaka wa 2013 aliyekuwa Rais Mhes. Kibaki wa chama cha PNU alikuwa anastaafu. Waliotafuta uongozi ni aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga wa ODM nao mrengo mwingine wa Mhes. Uhuru Kenyatta wa TNA na William Ruto wa URP (IEBC, 2013). Walitumia hotuba katika mikutano kiujuzi kuwasisimua wafuasi, kuwasuta wapinzani na kuwazindua wananchi. Adero (2005) anaeleza kuwa, lugha katika hotuba hutumiwa na wanasiasa kuonyesha itikadi zao.

Utafiti huu ulinuia kuonyesha jinsi vipengee vya wakaa, uwasilishaji wa usemi na wahusika vinavyojitokeza katika hotuba hizi na dhima zake. Hotuba haijafanyiwa uchunguzi wa kina kimtindo kwa kurejelea nadharia ya Naratolojia. Isitoshe, hakuna

uhakiki wowote ambao umefanywa kuhusu tanzu za fasihi simulizi kwa kurejelea mawazo ya Rimmon-Kenan.

## 1.1 Suala la Utafiti

Suala la usimulizi limeshughulikiwa na watafiti mbalimbali kwa mikabala tofauti. Tafiti za Mulama (2011), Khamisi (2015) Muiya (2018), Kinga (2022) miongoni mwa zingine zilishughulikia usimulizi katika riwaya na tamthilia. Kwa upande mwingine, usimulizi katika utenzi kama kitanzu cha ushairi ulichunguzwa na Arege (2012) huku uzingativu ukiwa kwenye vipengele vya wakati, daraja ya sauti na uhusika. Utafiti wa Kwaka (2012) uliangazia vipengele vya wakati na uwasilishaji wa usemi katika *Utenzi wa Nabii Issa.* Ni bayana kuwa tafiti hizi zilijikita katika uwanja wa fasihi andishi. Aidha, tafiti zilizofanywa kuhusu hotuba ni za Jagero (2015), Lwaitama (1988), Adero (2005) na Musa (2015) na zilijikita katika uchanganuzi wa lugha itumiwayo, maudhui na mtindo bila kurejelea mtindo wa usimulizi. Kwa mujibu wa upekuzi wa undani wa mtafiti, hakuna utafiti wa kina ambao umefanywa kuhusu usimulizi kwa misingi ya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba za wanasiasa wa Kenya. Kwa hivyo, utafiti huu ulihusu ubainishaji wa vipengee vya wakaa, uwasilishaji wa usemi na wahusika katika hotuba teule za Uhuru Kenyatta, William Ruto na Raila Odinga.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

i. Kubainisha jinsi kipengele cha wakaa kimetumiwa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.
ii. Kudhihirisha jinsi wahusika wanavyojitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

iii. Kubainisha jinsi kipengele cha uwasilishaji wa usemi kimejitokeza na kujadili dhima ya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulitarajiwa kujibu maswali yafuatayo:

a) Je, ni kwa jinsi gani kipengele cha wakaa kimejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya?

b) Je, wahusika wanajidhihirisha vipi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya?

c) Ni kwa jinsi gani kipengele cha uwasilishaji usemi kinajitokeza na dhima zipi zinawasilishwa na vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika kuwasilisha dhamira ya wanasiasa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya?

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Hakuna tafiti nyingi kufikia sasa ambazo zimechunguza usimulizi katika tungo za fasihi simulizi. Nyingi yazo ziliegemea utenzi kama vile ule wa Arege (2012) na Kwaka (2012). Asige (2021) alichunguza usimulizi katika nyimbo. Pengo lilibainika la kuchunguza usimulizi katika hotuba ambalo utafiti huu ulinuia kuliziba.

Aidha, utafiti huu ulichunguza usimulizi katika hotuba kwa mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002) kinyume na tafiti za Arege, Kwaka na Asige (wameshatajwa) ambao walizingatia mawazo yake Genette (keshatajwa). Rimmon-Kenan (2002) aliendeleza na kuboresha mawazo yake Genette (keshatajwa) kwa kuibua kipengele cha hadithi, matini na usimulizi. Matini ilihusisha wakaa, wahusika na sauti ya usemi kinyume na vipengele vyake Genette (1980) aliyeonyesha vipengele vya sauti, wakati na hali. Hivyo, utafiti huu ulivirejelea vipengele vyake Rimmon-Kenan katika hotuba.

Halikadhalika, utafiti huu umeziba pengo ambalo liliachwa na wahakiki ambao walishughulikia hotuba. Musa (2015), Matasi (2014), Jagero (2015), Mahadi (2001), Elia (1989) na wengi waliochunguza maendeleo ya hotuba, maudhui, lugha na mtindo kwa kuangalia tamathali za usemi bila kuzingatia usimulizi. Utafiti huu umeziba mwanya huu kwa kuzingatia malengo tofauti.

Wanasiasa walioteuliwa kuhakikiwa, hotuba zao hazijafanyiwa utafiti wa aina hii. Hili lilitupa shime ya kuzamia katika utafiti huu ili kuweka bayana suala la usimulizi katika hotuba linavyosaidia kuelewa maandishi bila kuhusisha na muktadha.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulichunguza wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hotuba zilizoteuliwa ni kauli walizotoa zisizo rasmiwakati wa kampeni za kisiasa wanasiasa Mhes. Kenyatta, Mhes. Odinga na Mhes. Dkt. Ruto zilizotolewa mwaka wa 2013 hadi 2023. Wao ni wanasiasa maarufu nchini kulingana na takwimu za Tume ya Uchaguzi nchini (IEBC). Uchaguzi wa 2013 Kenyatta (TNA) alikuwa na kura 6, 173, 433 naye Odinga (ODM) 5, 340, 546. Uchaguzi wa 2017 Kenyatta (JP) alipata kura 8, 203, 290 naye Odinga (ODM) 6, 762, 224 katika uchaguzi wa 2022 Ruto (UDA) alipata kura 7, 176, 141 naye Odinga (ODM/ Azimio) 6, 942, 930. Hotuba zilizoteuliwa zenye data lengwa zilizingatia kipindi hiki na zililenga masuala ya kampeni za kisiasa pekee.

Isitoshe, suala zima la usimulizi huhusu vipengele vingi ambavyo haviwezi kuchanganuliwa katika utafiti mmoja. Hii ilikuwa sababu ya kuchagua vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika kutumika ili kudadavua usimulizi katika hotuba na dhima yavyo katika kuwasilisha dhamira ya wanasiasa.

Utafiti ulielekezwa na nadharia ya Naratolojia kwa mawazo ya Rimmon-Kenan (2002). Mtazamo wake ulitumika kuchanganua vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule na kuonyesha dhima ya vipengee hivi.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Yaliyoandikwa kuhusu mada yaligawanywa katika sehemu mbili: tafiti zinazohusu usimulizi na tafiti zinazohusu hotuba.

#### 1.6.1 Tafiti Zinazohusu Usimulizi

Muiya (2018) alifanya utafiti kuhusu muundo wa simulizi katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya ya *Vute N'kuvute* yake Adam Shafi. Alionyesha kuwa vipengele vya hadithi, matini na usimulizi vimejitokeza kiuamilifu katika kuijenga riwaya aliyohakiki. Alidhihirisha usawiri wa wahusika wa moja kwa moja, akaonyesha kujitokeza kwa analepsia na prolepsia pamoja na vipengele vya wakaa. Kazi yake ilimwezesha mtafiti kuelewa mtazamo wake Rimmon-Kenan (2002) kuhusu Naratolojia japo huu ulihusu hotuba.

Kwaka (2018) alichunguza usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Issa*. Aligusia vipengele vya wakati na uwasilishaji usemi. Alionyesha kuwa mpangilio wa matukio katika utenzi huo haukutumika kiukamilifu kwa mtunzi kutumia kipengele kimoja analepsia kuliko prolepsia. Utafiti huu unaonyesha vipengele hivi vimetumika kikamilifu. Alibainisha pia mbinu za uwasilishaji usemi zilizotumika. Utafiti wake ulimfaa mtafiti katika kuelewa kipengele cha uwasilishaji usemi licha ya kuwa alishughulikia utenzi katika mkabala wa Genette (1980).

Mulama (2011) alitafiti kuhusu usimulizi katika Utenzi wa *Siri Li Asirali*. Aligusia vipengele vya aina ya wasimulizi, sifa za usimulizi, kuonekana kwa usimulizi, utegemefu wa usimulizi na hadhi ya mtazamo katika usimulizi. Alichunguza kipengele cha wakati, kwa hivyo utafiti wake ulifaa utafiti huu kwa kutoa mwelekeo kuhusu wakaa japo hapa tulijibana katika hotuba. Mawazo yake yalijikita katika mtazamo wa Rimmon-Kenan (2002), malengo yake ya utafiti yanatofautiana na ya utafiti huu.

Uhakiki wa usimulizi katika riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi uliofanywa na Ong'ondi (2005) ulichunguza vipengele vya wakati na mtazamo kwa kuangalia tofauti zilizopo. Alionyesha jinsi aina za usimulizi zilivyodhihirika. Alijadili uwasilishaji wa usemi kama unenaji kwa kuonyesha kuwa usemi wa nafsi ya tatu ulijitokeza kwa uchache. Utafiti huu kuhusu kipengee hiki katika hotuba ulionyesha kuwa usemi wa nafsi ya tatu hujitokeza kwa wingi kinyume na mawazo yake. Mawazo yake yaliufaa utafiti huu japo ulishughulikia hotuba.

Uhakiki wa simulizi bunilizi katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ulichambua wakati, wahusika, mtazamo na uwasilishaji usemi na mawazo. Kimani (2012) alionyesha kuwa mbinu za uwasilishaji usemi zilithibitishwa bila uwepo wa uwasilishaji wa mawazo. Utafiti huu ulionyesha haya yapo. Utafiti wake ulimfaa mtafiti kwa kumwezesha kuelewa kuhusu nadharia ya Naratolojia.

Asige (2021) alichunguza usimulizi kama mtindo katika nyimbo za Bahati Bukuku. Aliangalia mfuatano wa matukio, wakati, maudhui, sauti ya usimuliaji na mahusiano ya wakati wa usimulizi. Alionyesha utangulizi maalum hufanikisha uwasilishaji wa simulizi. Nafsi iliyotawala katika nyimbo hizo ilikuwa ya mhusika mkuu. Japo utafiti

wake uliufaa utafiti huu, tofauti ni kuwa alilenga mawazo yake kwa mtazamo wa Genette (keshatajwa) ilhali huu ulijikita katika mawazo yake Rimmon-Kenan (keshatajwa).

### 1.6.2 Tafiti Zinazohusu Hotuba

Uchunguzi kuhusu uwezo wa lugha katika matini ya siasa nchini Kenya mwaka 2002 hadi 2005 ulifanywa na Adero (2005). Alilenga kuonyesha vile lugha hutumiwa na wanasiasa kuonyesha itikadi zao. Alidhihirisha kuwa wanasiasa wana lugha isiyo wazi na uneni wao hutumia lugha pinde unaowafanya kupata wafuasi wengi. Alisema lugha ina dhima ya kuzindua, kutahadharisha, kutoa ahadi na matumaini. Kinyume na utafiti wake, utafiti huu ulishughulikia uhakiki wa mtindo wa usimulizi.

Musa (2015) alichanganua hotuba za Mwalimu Nyerere kwa mkabala wa nadharia ya Balagha. Alichunguza maudhui mahususi na kubaini yale ya umoja wa kitaifa, Azimio la Arusha, uongozi bora, demokrasia na elimu kwa wote. Aidha, alichunguza mbinu za kiisimu zinazozua ushawishi, utafiti huu ulimfaa mtafiti kwani ulishughulikia utanzu ambao huu ulitafiti: hotuba. Tofauti ni kuwa huu ulishughulikia usimulizi kama mtindo ilhali yeye aliguzia mtindo kwa kudondoa vipengee tofauti pamoja na maudhui.

Lwaitama (1988) alichunguza Hotuba za kisiasa katika Kiswahili: mtindo wa maongezi ya wanasiasa wa Tanzania (Nyerere na Mwinyi). Alionyesha kuwa utumiaji wa viwakilishi nomino hutegemea muktadha. Alionyesha walitumia nafsi ya kwanza katika maongezi kuliko katika matini iliyoandikwa. Akaongeza kuwa viongozi hawa walitumia nafsi ya pili walipotaka kuunda Jumuiya ya Tanzania. Alichunguza pia mwingiliano katika usemi. Utafiti huu ulishughulikia mtindo wa usimulizi, kipengee

mahususi kinyume na utafiti wake uliongalia kijumla, nadharia aliyoitumia (uhakiki changanuzi wa lugha) ni tofauti na ile huu ulitumia (Naratolojia).

Tafiti nyingi kuhusu hotuba zimeshughulikia lugha, maudhui na mtindo. Zilizofanywa kuhusu usimulizi ziliegemea vipera vingine vya fasihi simulizi kama vile nyimbo kwa mikabala ya wananaratolojia wengine kama Genette. Hivyo kutokana na uchunguzi pevu wa mtafiti, hakuna utafiti umefanywa kuhusu mtindo wa usimulizi katika hotuba za kisiasa. Pengo hili limezibwa na utafiti huu.

### 1.7 Msingi wa Nadharia

Wamitila (2003) anasema kuwa msingi wa mawazo ya nadharia hii ni mwanafalsafa Plato katika *The Republic*. Anaeleza kuwa usimuliaji huhusu mimesia: mtunzi wa fasihi hajitokezi wazi kama mnenaji na daijesia ambapo mtunzi hujitokeza na kujulikana kama mnenaji. Mwanafunzi wake Aristotle aliyaendeleza mawazo haya katika *The Poetics* kwa kuhusisha dhana hizi na uelezaji.

Nadharia hii ilihusishwa na kazi za urasimu wa Kirusi za mtaalamu Vladmir Propp (1968) aliyefanya tafiti kuhusu hurafa za kirusi na kuchapisha kitabu cha *Morphology of the Folktale.* Pia*,* Lord Raglan (1956) alichunguza visasili katika jamii mbalimbali. Visasili hivi ni kama Robin Hood, Oedipus, Moses na wengine. Alichapisha kazi yake *The Hero* iliyosema kuwa kuna mfuatano maalum wa matukio: kabla shujaa azaliwe, kuzaliwa kwake hutabiriwa, kutanguliwa na mambo ya ajabu katika jamii, kuwa na jaribio la kuuliwa, kutoroka kwao na kurudi kuiokoa jamii yake. Wengine ni wataalamu wa anthropolojia muundo kama Roland Barthes (1970) aliyeandika kitabu *"An Introduction to The Structural Analysis of Narratives"* kinachosema kuna aina za

simulizi na tanzu zilizogawanyika katika njia za uwasilishaji: kuongea kimaandishi au kimapokeo, ishara na picha.

Gerard Prince anasema kuwa Naratolojia ni stadi ya aina na utendaji kazi wa simulizi. Haijishughulishi na historia ya thamani na ujumi bali sifa zinazobainisha simulizi, mifumo na mitindo ya sifa hizi. Naratolojia huangalia undani wa vifaa vinavyoongoza maelezo ya simulizi na ufahamu wa utendaji kazi wake (Prince, 1982:5). Anahusisha simulizi na anayesimulia "mimi", hadhira inayosimuliwa "wewe" na hadithi "yeye" kudhihirisha uwasilishaji wa usemi. (Kwaka, 2018) anasema kuwa, haya yamejadiliwa pia na Landa (1990) katika kitabu chake *Narrative Theory.*

Gerard Genette (1980) katika kitabu chake *Narrative Discourse* alieleza Naratolojia kwa kuigawa katika mambo matatu; simulizi: kauli inayotumiwa kuelezea tukio, hadithi: mfuatano wa matukio ya kibunilizi au halisi na usimuliaji ambao ni tendo la kusimulia. Kumaanisha kuwa simulizi hutamba tukio, ni maelezo bali sio masimulizi (Kinga, 2020).

Mieke Bal (2009) anasema Naratolojia hujihusisha na simulizi, matini zake zenye picha na huhusisha matendo na vifaa vya kitamaduni kuelezea hadithi na kuhakiki simulizi kiundani kwa kurejelea sifa zinazoambatanishwa na simulizi na kuweka kando zisizohusiana yaani matini kufuata kanuni maalum.

Utafiti huu umerejelea mawazo yake mtaalamu Rimmon-Kenan (2002) ambaye alinuia kuimarisha mawazo ya Genette (1980) kwa kupanga vipengele vya usimulizi jinsi vinavyohusiana na kutegemeana. Vipengele hivyo ni hadithi, matini na usimulizi.

Matini ilihusisha wakaa ilhali kile cha usimulizi kikihusisha sauti. Vipengele vingine ni uhusika na wahusika pamoja na uwasilishaji wa usemi.

Msingi wa mawazo yake ni vipengele vilivyotumika katika kuhakiki usimulizi kama mtindo katika hotuba. Hivi ni mihimili mikuu itakayotumika katika utafiti huu. Mihimili hiyo ni wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika. Anaeleza wakati kama mpangilio wa matukio katika hadithi (Rimmon-Kenan, 2002:44). Ni vipindi ambapo hali na matukio yanasimuliwa na uwasilishaji wake hutokea; kipindi cha kihistoria ambacho msingi wake ni kazi husika (Wamitila, 2003:348). Genette na Rimmon-Kenan wanazua dhana za wakati hadithi kuonyesha wakati unaochukuliwa na hadithi kutoka mwanzo hadi mwisho kama saa, siku, wiki, mwezi au miaka. Aidha, wanazua dhana nyingine ya wakati matini inayorejelea wakati unaochukuliwa na msomaji kuisoma hadithi. Kipengele hiki huwa na vigezo vya mpangilio, muda na idadi marudio vilivyojadiliwa katika utafiti.

Kipengele cha uwasilishaji wa usemi kinaonyesha jinsi maana hutolewa mhusika anapotumia lugha. Huhusu daijesia na mimesia. Haya pia yalichambuliwa kwa kina katika kazi hii. Wahusika ni viumbe au vitu ambavyo hutumiwa na msimulizi kuwasilisha ujumbe. Utafiti ulionyesha jinsi wanavyosawiriwa na wanasiasa.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inahusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo kutokana na uchanganuzi wa data.

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulichukua muundo wa kimaelezo kwa kueleza yaliyomo. Mtafiti alichunguza jambo katika jamii bila kuingiliana kwa kupitia maandiko kuhusu suala hilo. Mkabala huu ulitegemea ushahidi uliyomo katika vitabu, majarida, magazeti, tawasifu, tasnifu, video na vyombo vya kunasa sauti.

Mtafiti alizingatia kile alichotafiti kulingana na suala la utafiti, kujua aina ya hifadhi ya mambo aliyotaka kama vitabu, majarida, video za hotuba mtandaoni *YouTube* na magazeti, aliibua mfano wa kuainisha habari alizochuja kutoka kila hifadhi kama hotuba – usimulizi – wakaa – muda na kudondoa Ushahidi.

Mkabala wa kithamano ulirejelewa kwani data iliyokusanywa sio ya kitakwimu na utanzu huu huwasilishwa kwa usemaji. Sababu za mkabala huu kuchaguliwa ni kuwa utafiti huu ulifanikishwa na njia za ukusanyaji data kama maelezo na uchanganuzi kwa kurejelea nadharia ya Naratolojia kwa mawazo yake Rimmon-Kenan (2002).

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyikia maktabani. Maktaba ya chuoni, mtandao wa *YouTube*, maktaba za mashirika ya habari na Makavazi ya Kenya. Mtafiti alisoma makala kuhusu nadharia ya Naratolojia, tasnifu na makala kuhusiana na mada ya usimulizi. Alisoma magazeti, akasikiza rekodi za hotuba za wanasiasa teule tokea mwaka 2013 hadi 2023. Haya yalisaidia kutoa maelezo na maelekezo ya jinsi ya kuufanya utafiti huu.

### 1.8.3 Sampuli na Usampulishaji

Usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa kama mbinu katika utafiti huu kwa sababu sampuli iliyotakikana ilikidhi malengo ya utafiti. Ulimwezesha kuchagua sampuli

yenye sifa zenye wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Aidha, mbinu hii iliokoa muda na gharama za utafiti.

Sampuli ya msingi katika utafiti huu ni wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule tatu kwa kila mwanasiasa rejelewa. Hotuba hizi ni zile zenye data utafiti huu ulichunguza. Wanasiasa watatu Kenyatta, Odinga na Ruto walirejelewa. Walichaguliwa kwa kuwa kauli zao zilitimiza malengo ya utafiti na ni wenye umaarufu (IEBC, 2013).

### 1.8.4 Ukusanyaji Data

Mbinu za utazamaji, usikilizaji na uchanganuzi matini zilitumika kujenga na kusaidia kupata data ya kweli. Balnaves na Caputi (2001: 103) wanasema kwamba wanataaluma wa kisasa wa sayansi ya kijamii hutumia mbinu zaidi ya moja za ukusanyaji data ili kupata habari ambazo hazina kiwango kikubwa cha upendeleo.

Jambo la kwanza ambalo mtafiti alifanya ni usampulishaji kulingana na malengo ya utafiti kabla ya kuchagua hotuba zilizotumika. Mtafiti aligeuza kanda za sauti na video hadi mfumo wa maandishi ili kurahisisha ukusanyaji wa data zilizofaa kulingana na maswali na malengo ya utafiti.

Uchanganuzi matini ulihusu kupitia yanayohusiana na mada ya utafiti kwa kusoma makala kuhusu usimulizi, nadharia ya Naratolojia na tasnifu husika. Magazeti na makala yenye hotuba za wanasiasa lengwa yalirejelewa.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data ilichanganuliwa kimaelezo baada ya kusomwa na kusikizwa kwa makini hotuba teule. Data ichangunuliwayo kimaelezo huwekwa katika sehemu ndogo kumwezesha

mtafiti kuwasilisha kwa kifupi (Mutugu, 2019). Utafiti ulizingatia maswali, malengo na mihimili ya nadharia ya Naratolojia. Kwanza mtafiti alikusanya data maktabani kwa kusoma makala kisha akatazama video za *YouTube*.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo yalitolewa kwa njia ya maelezo kwani ulihusu kufasili matini zilizomo. Maelezo yalitolewa kulingana na malengo ya utafiti ili kujibu maswali ya utafiti huu kwa kutumia data za kiuthamano kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Naratolojia iliyotumiwa kuchunguza usimulizi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

## 1.9 Maadili ya Utafiti

Utafiti huu haukuwa wa kitakwimu, uligusia maisha ya wanasiasa lengwa. Hivyo, ilimbidi kuwaheshimu na kuheshimu maoni yao kuhusu yale ambayo walikuwa wanayapigania katika hotuba zao. Ili kuheshimu kazi za watafiti na wataalamu wengine ambazo zilirejelewa, mtafiti amewanukuu ili kuonyesha kuwa si mawazo yake bali yao. Ilipohitajika, aliomba ridhaa yao na kujenga uhusiano nao.

Mbali na hayo mtafiti alijukumika kupata vibali hitajika kabla ya kuingia nyanjani na kuzama katika utafiti. Alitafuta vibali kutoka kwa shule husika, kitengo cha *Center for Research Ethics and Safety (CRES)* pamoja na *National Council for Science and Technology and Innovation (NACOSTI).*

# SURA YA PILI

# WAKAA KATIKA HOTUBA TEULE ZA WANASIASA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imebainisha jinsi kipengele cha wakaa kimetumiwa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa wakaa ni kipengele kinachoonyesha uhusiano wa kimfuatano kati ya hadithi na matini. Anakiainisha katika wakati hadithi ambacho ni kipindi hadithi nzima huchukua kutoka mwanzo hadi mwisho kwa mfano: saa, siku, juma, mwezi au miaka na wakati matini ambacho ni kipindi au wakati anaouchukua msomaji kusoma matini fulani. Genette (1980) anasema kuwa wakaa ni kipindi cha muda maalum wa kufanya jambo fulani. Kinga (2020) anasema ufafanuzi wa Genette (1980) unaegemea matini ya kifasihi kinyume na muda utumikao kutamka sauti yoyote katika sarufi. Kwa hivyo, wakaa ni muda unaotumika kuendeleza matukio katika fasihi. Kipengele hiki ndimo wahusika huishi, matukio kufanyika na maudhui kujitokeza (Khamis, 2015).

Utafiti huu ulichunguza namna wanasiasa teule walivyosimulia jambo la kipindi fulani katika hotuba zao. Utafiti huu ulichanganua vipengele vya wakaa vya umara/ idadi ya utokeaji wa matukio, muda na mpangilio. Muiya (2022) katika utafiti wake anasema hivi ni vigezo vinavyotumika kuonyesha uhusiano kati ya wakati hadithi na wakati matini. Vipengele vya umara, muda na mpangilio vilichunguzwa kwa kutolewa mifano jinsi vinavyojibainisha katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya (Kenyatta, Raila na Ruto).

## 2.1 Mpangilio

Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa mpangilio wa matukio ni mfululizo wa matukio ya kihadithi na jinsi yanavyochangia kuelezea maana na hisia. Aidha, anasema kuwa wakaa ni uhusiano wa mtiririko wa matukio baina ya hadithi na matini. Hutoa maelezo ya awali kuhusu mhusika au tukio kutokana na masimulizi yanayotolewa wakati huo. Genette (1980) anaeleza kuwa ni uhusiano baina ya mfuatano wa matukio katika hadithi. Kinga (2020) anasema kuwa mpangilio wa matukio hulenga kujibu swali lini tukio lilitokea kabla au baada ya wakati wa usimulizi. Mpangilio wa matukio ni kipengele kinachoonyesha jinsi matukio yamefuatana kwenye hadithi kwa kuzingatia au bila kuzingatia wakati.

Masimulizi ya matukio yanavyotokea kiwakati huwa ni mpangilio wa kiwakati ilhali matukio yanaposimuliwa bila kuzingatia wakati huwa ni anakroni (Genette, 1980) hurejelea jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka; yanapofuatana moja baada ya jingine yanaposimuliwa kiwakati (Wamitila, 2002) au tukio lililopaswa kutangulia husimuliwa baadaye katika masimulizi, mbinu iitwayo analepsia au tukio la mwisho kujitokeza mwanzoni mbinu iitwayo prolepsia.

Rimmon-Kenan (1983), Genette (1980) na Jahn (2005) wanakubaliana kuwa analepsia (mbinu rejeshi/ kisengere nyuma) na prolepsia (mbinu elekezi/ kiangaza mbele/ ubashiri) ni aina mbili kuu za anakroni. Utafiti huu ulidhihirisha matumizi ya mbinu hizi mbili za anakroni katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

### 2.1.1 Analepsia

Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa analepsia ni usimulizi wa hadithi ambapo tukio la mbele linasimuliwa kabla ya yale yaliyotendeka kabla yake. Wamitila (2003:117)

anaeleza kuwa mbinu rejeshi (analepsia) hutumiwa na waandishi kuelezea matukio yaliyotokea nyuma ya wakati wa hadithi. Muiya (2022) katika tasnifu yake anasema kuwa hii ni mbinu inayoeleza yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. Kwa hivyo, analepsia ni mbinu ambayo matukio ya awali au yaliyofanyika kitambo yanarejelewa katika matini au masimulizi ya matukio yanayofanyika sasa au yalifanyika baada ya hayo kufanyika.

Rimmon-Kenan (keshatajwa) anatambulisha aina za analepsia kwa kuzingatia kigezo cha anayesimulia na sehemu ya simulizi inayorejelewa. Aina hizi ni analepsia tawasifu, analepsia wasifu, analepsia ya nje, analepsia ya ndani.

#### 2.1.1.1 Analepsia Tawasifu

Genette (keshatajwa) anasema hii ni aina ya analepsia ambayo hutoa maelezo kuhusu mhusika, tendo au simulizi ya tukio la awali katika simulizi ya tukio. Khamis (2015) katika tasnifu yake anaeleza kuwa ni analepsia ambayo hutoa taarifa juu ya tukio lililopita au mhusika anayesimuliwa au tukio au hadithi. Analepsia tawasifu hutoa taarifa zaidi ya kale kumhusu mhusika au tendo fulani linalosimuliwa. Aina hii inadhihirika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya zinazoshughulikiwa.

Katika hotuba yake Rais Mstaafu Kenyatta aliyotoa katika mkutano wa kampeni za urais mwaka 2017 katika uwanja wa Afraha – Nakuru, anasimulia jinsi alivyoanza siasa zake na Mhesh. Ruto mwaka 2013. Anasema hivi:

> Sasa wakati tulianza siasa, tulizianzia hapa Afraha. Mimi na huyu ndugu yangu kijana William Ruto. Tukakuja hapa tukawauliza wenzetu wa Nakuru sisi tungependa tuungane pamoja na kupitia siasa tuweze kuhubiri amani, tuweze tuhubiri umoja na ndio tena Mkenya asimwage damu yake, asipoteze mali yake kwa sababu ya siasa.

Kauli hii ni analepsia tawasifu, anasimulia jinsi walivyoutangaza muungano wao kule Nakuru wa kinyang'anyiro cha kuwania urais. Tukio hili lilifanyika mwaka 2013 kabla ya wakati wa sasa; mwaka 2017 ambapo wamerudi tena kuomba kura. Mbinu hii inatusaidia kuelewa jinsi wapiga kura wa Nakuru ni muhimu kwa ushindi wao na jinsi muungano wao ulivyosaidia kuzuia vita vya baada ya uchaguzi kama vile ilivyofanyika mwaka 2007. Tukio la vita vya baada ya uchaguzi lilifanyika kitambo lakini analirejelea kwa kusema wanahubiri amani ili kuzuia umwagaji damu. Sifa ya wanasiasa kujitapa na kuhubiri amani katika kampeni inajitokeza.

Anaendelea kusema:

> Wenzetu, kwa muda mchache sana wa miaka minne, tumeweza kuongeza idadi ya Wakenya ambao tulipata wakiwa milioni mbili ambao walikuwa wameunganishwa kwa huduma ya stima, tukaongeza idadi ya Wakenya kwa milioni sita elfu mia tano.

Matukio haya yalifanyika zamani kabla ya wakati wa masimulizi. Anayarejelea ili kujipigia upato kwa kuonyesha maendeleo ambayo ameyafanya na jinsi mambo yalivyokuwa kabla kuteuliwa kama rais ili kuwashawishi wapigaji kura kumteua tena kama rais.

Analepsia tawasifu inajitokeza pia katika hotuba yake Mhes. Ruto anayoitoa huko Nakuru tarehe 2/10/2021. Anasema:

> Leo nimefika hapa Nakuru ili tuweze kukubaliana vile tunaenda mbele pamoja. Tulikuja hapa na rafiki yangu rais wa Jamhuri ya Kenya na tukawaambia watu wa Nakuru ya kwamba tunaanzisha safari ya kuunganisha Kenya na kuondoa siasa ya chuki, ukabila na migawanyiko ili Kenya tuweze kuiunganisha, tuunganishe jamii zote, tuunganishe sehemu zote za Kenya na tuunde serikali ambayo *itatransform* nchi ya Kenya kupitia kwa mipango ya miradi na sera ya maendeleo.

Katika kauli hii, Mhes. Ruto anarejelea tukio lililofanyika mwaka wa 2013. Anaeleza jinsi walivyohubiri amani na kuwaunganisha wakenya ndiposa wakaweza kuchaguliwa. Dondoo hili linaonyesha jinsi suala la amani ni muhimu katika kampeni za wanasiasa. Ni sera muhimu kuuzwa kabla ya kuuza sera yoyote ile nyingine kwa wafuasi wao. Inajitokeza pia katika hotuba yake Mhes. Odinga, hotuba aliyoitoa katika mkutano wa siasa Uhuru Park mwaka wa 2017. Anasema:

> Leo, wale ambao walikuwa na tashwishi watajua kuna tsunami. Nilisema tsunami itakuja. Imeanza leo, kuelekea tarehe nane. Nane, nane, nane, ni nane mara tatu.

Odinga anarejelea kauli aliyotoa katika mkutano wa siasa mwaka 2016 kuhusu muungano ambao wangeunda kupigania urais katika uchaguzi wa mwaka 2017. Kauli hii inaonyesha jinsi wanasiasa husisitiza ujumbe kwa kurudia rudia kile walichosema katika harakati zao za kutafuta uungwaji mkono.

#### 2.1.1.2 Analepsia Wasifu

Hii ni aina ya analepsia ambayo hutoa taarifa kuhusu matukio yaliyopita kumhusu mhusika mwingine au tukio jingine ambalo halihusiani na kile kinachosimuliwa au kurejelewa kwa hadithi inayosimuliwa wakati huo. Huhusu masimulizi kukatizwa na na yale ya kitambo kumhusu mhusika mwingine au tukio jingine kuingizwa. Aina hii imejitokeza katika hotuba zilizoteuliwa za wanasiasa wa Kenya. Katika hotuba yake aliyoitoa kule Nakuru mwaka 2017, Mhes. Kenyatta anabadili mwelekeo wa kusifu yale ambayo serikali yake imefanya na kumsuta mpinzani wake kwa kupinga miradi ambayo serikali yake ilikuwa ikiendeleza. Anasema:

> Mwenzangu ambaye twashindana naye akasema, “angalia hawa watu ati wanapatia stima, wanawaekea nyumba ya nyasi stima.” Huyo ndio mtu wa kitendawili na anasema kwa mkutano wa hadhara.

Dondoo hili linadokeza wazi wajibu wa wanasiasa. Wale ambao wako katika upinzani ni kupinga baadhi ya mipango ya serikali ambayo wanahisi haiwafai wananchi kwa kuonyesha upungufu wake ili kujipigia upato na wale walio serikalini ni wajibu wao kusema yale ambayo wameyafanya ili kupewa nafasi nyingine ya kuliongoza taifa. Mkondo wa masimulizi umebadilika kwa kuacha yale aliyokuwa anayasimulia kwa kumwingilia mpinzani wake kwa yale aliyoyasema kitambo.

Analepsia wasifu inajitokeza pia katika hotuba yake Mhes. Ruto aliyoitoa huko Nakuru mwaka 2021, anasema:

> Lakini hawa wageni waliotutembelea walituletea mambo ya BBI na Reggae. Nataka kuwaambia watu wa Nakuru, hio BBI ilikuwa ya ulaghai zaidi, mojawapo ya mpango wa udanganyifu kuwahi kufanywa na utawala wowote.

Hii ni analepsia wasifu kwani anarejelea tukio lililopita kuhusu mswada wa BBI katika masimulizi yake ya kukipigia chama cha UDA umaarufu. Kupitia kauli hii anawafahamisha wafuasi wake kuhusu upungufu wa mswada huo na sababu za kutokuwa mzuri kwa wananchi. Inajitokeza katika hotuba yake Mhes. Odinga. Anasema:

> Kule Tanga mjini kule Tanzania, Rais Magufuli na Rais Museveni wanazindua ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka bandari ya Tanga Tanzania. Huo ni urefu wa kilomita elfu moja mia nne hamsini, lakini kutoka Hoima mpaka Mombasa ni kilomita mia tisa hamsini pekee yake. Ile ya Tanzania ni ndefu kwa kilomita mia tano zaidi lakini Museveni amesema hawezi kupitisha Kenya kwa sababu ya ufisadi.

Kupitia dondoo hili, ananuia kudhihirisha ufisadi uliyomo katika serikali na kuwapa wafuasi wake sababu ya kuitoa uongozini na kupewa nafasi ya kuliongoza taifa. Amerejelea tukio ambalo lilifanyika kule Uganda, hii ni analepsia wasifu.

#### 2.1.1.3 Analepsia ya Nje

Wamitila (2003) anasema hii ni mbinu ya usimulizi inayohusisha matukio ambayo yako nje ya wakati wa mwanzo wa hadithi. Genette (1980) anasema ni masimulizi ya matukio ya kabla ya kuanza kwa hadithi. Analepsia ya nje ni masimulizi ya jambo lililofanyika kitambo kabla ya yale yanayosimuliwa hadithini. Inajitokeza katika hotuba yake Mhes. Ruto mwaka 2019 anaposema:

> Ile siasa ya zamani ya ugomvi na chuki, na fitina na mambo ya ukabila. Tumesema hio siasa haina nafasi katika Kenya ya karne ya ishirini na moja.

Hapo, huenda anadhihirisha jinsi siasa za Kenya zilivyokuwa baada ya kujinyakulia uhuru hadi karne ya ishirini. Masimulizi yake na kampeni zake zinafanyika katika karne ya ishirini na moja. Anadhihirisha maudhui ya ukabila kwa kuonyesha jinsi siasa ilivyokuwa wakati huo. Rais Kenyatta pia anasema:

> Na tukasema wakati huo 2013. Tukasema tushinde au tushindwe, sisi haja yetu ni ya amani na Wakenya waishi pamoja.

Katika kauli hii, anarejelea hotuba aliyoitoa mwaka wa 2013 katika kampeni kule Nakuru. Hii ni analepsia nje kwani katika simulizi yake ya kinyang’anyiro cha urais mwaka 2017, anarejelea simulizi ya 2013 ambayo ni tofauti na aliyokuwa anatoa. Hii ni analepsia ya nje inayodhihirisha sababu yake kujiunga na Mhes. Ruto kutafuta urais mwaka huo.

#### 2.1.1.4 Analepsia ya Ndani

Wamitila (2003) anasema kuwa ni mbinu rejeshi ambayo huhusisha matukio yaliyopita lakini yasiyokuwa ya kabla ya wakati ianzapo hadithi. Asige (2021) anasema ni masimulizi ya matukio yanayotokea baada ya kuanza hadithi lakini hayasimuliwi wakati yalipotendeka. Ni yale yanayofanyika kabla ya masimulizi kuanza na husimuliwa baadaye katika hadithi. Inajitokeza katika hotuba yake Mhes. Odinga ambapo anakatisha masimulizi yake na kuwaeleza wafuasi wake kuwa miongoni mwao kuna aliyekuwa rais wa Afrika Kusini Thabo Mbeki. Tukio hili halifanyiki wakati huo anapowasili bali alikuwepo wakati masimulizi yalipoanza lakini tukio halikujitokeza. Anasema:

> Tuko hapa na aliyekuwa rais wa Afrika Kusini, South Africa, Mhes.
> Thabo Mbeki yuko hapa, amekuja kushuhudia uchaguzi.

Ujio wake haujajitokeza mwanzoni mwa masimulizi (hotuba) yake bali unajitokeza katikati mwa masimulizi yake kabla ya kumalizia kuuhutubia umati uliokuwepo.

#### 2.1.1.5 Analepsia Mseto

Rimmon-Kenan (1983) anasema hii ni simulizi ya matukio yaliyotokea kabla ya simulizi ya mwanzo na kuendelea hadi mwanzo mwa simulizi au hata kuvuka mwanzo wa simulizi hiyo. Msimulizi hurejelea ya kale kabla ya mwanzo wa simulizi na kuyaunganisha na mwanzo wa simulizi anayosimulia. Inajitokeza katika hotuba yake Mhes. Ruto katika hotuba anayoitoa 2021 akikiuza chama cha UDA anapodhihirisha chanzo cha yeye kukianzisha chama hiki kwa kutoelewana na Mhes. Kenyatta kwa kukubali kushirikiana na chama cha upinzani ODM na kuwashirikisha viongozi wake katika serikali na kukisambaratisha chama cha Jubilee.

Anasema:

> Nyinyi mnajua tangu tupate mambo, tutembelewe na wageni, wale unawajua, tangu siku hiyo hatujapata amani, chama chetu cha Jubilee tulichotengeneza kwa misingi ya kuunganisha Wakenya. Leo chama hicho kimesambaratika kwa sababu wageni walitutembelea na wakasambaratisha chama chetu. Na kwa sababu hatutaki turudi tena katika siasa za ukabila na chuki, ndio tukaketi chini tukasema huo ujuzi tulitumia kuunda chama cha Jubilee kikawa chama cha kitaifa na tukatengeneza serikali nacho, ndio tutatumia safari hii, kutengeneza chama cha UDA.

Kutokana na analepsia mseto, suala la kale limedokezwa na kuonyesha jinsi linavyojenga suala la sasa linalosimuliwa. Ameweza kudhihirisha usaliti unavyojitokeza katika vyama vya kisiasa na jinsi wanasiasa hujituma kuanzisha vyama vipya baada ya kusalitiwa na wandani wao.

### 2.1.2 Prolepsia

Wamitila (2003) anasema kuwa hii ni mbinu ya kueleza hali ambapo mwandishi anatupa picha ya matukio ya mbele katika hadithi. Msimulizi hurejelea mambo ambayo yatafanyika baadaye katika simulizi ya sasa. Matendo yatakayotendeka baadaye yanasimuliwa mapema katika wakati ambao ni wa sasa na wakati wake haujafika.

Rimmon-Kenan (1983) anasema kuwa mbinu hii inapotumika huitoa taharuki inayotokana na maswali kama: nini kitafanyika baadaye? au mambo yanaenda kufanyika vipi? Aidha, anasema kuwa mbinu hii haifai kutumiwa kama kielelezo cha kukisia tukio la baadaye. Naye Toolan (1990) anasema kuwa mbinu hii huchujua taharauki ya hadithi kwa kusimulia matukio kabla ya ulazima wake kiwakati. Ni

mbinu ambapo matukio ya baadaye yanadokezwa kabla ya wakati wake wa kufanyika kufika, ya baadaye hurejelewa kabla ya sasa kusimuliwa.

Kulingana na Wamitila (2008), anasema kuwa baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa prolepsia hutumika zaidi katika kazi zilizosimuliwa katika nafsi ya kwanza kwani msimulizi huruka hadi matukio ya mbeleni. Utafiti huu umedhihirisha hotuba nyingi za wanasiasa hutolewa katika nafsi ya kwanza hasa katika wingi jinsi ilivyojitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

Utafiti huu ulibainisha kuwa prolepsia hutumika kwa wingi na wanasiasa katika harakati zao za kutoa ahadi na kutarajia uungwaji mkono kwani kwa kuwa ahadi hizo huhusu yatakayofanyika baadaye. Aina za prolepsia ni sawa na aina za analepsia. Hizi ni prolepsia mseto, ya ndani, ya nje, tawasifu na wasifu.

#### 2.1.2.1 Prolepsia ya Nje

Asige (2021) katika tasnifu yake anasema kuwa mtindo huu huhusu matukio ambayo yatatokea katika kipindi cha baada ya hadithi kusimuliwa na hayahitilafiani na hadithi ya kwanza. Wamitila (2008) naye anafafanua kuwa hadhira husimuliwa hadithi hadi mwisho bila kushuhudia tukio lililodokezwa kwani liko nje ya mipaka ya hadithi hiyo. Kwa hivyo, ni ubashiri wa yale yatakayofanyika baadaye lakini hayajitokezi au kufanyika popote katika simulizi rejelewa hadi mwisho wake. Mtindo huu umejitokeza katika hotuba ya Mhes. Odinga katika akiwa Bustani la Uhuru anaposimulia yale yangefanyika tarehe nane siku ya uchaguzi na yale ambayo yangefanyika tarehe tisa baada ya uchaguzi. Anasema siku hio wangepewa karatasi ya kura ambapo yeye kama mwaniaji jina lake na mgombea mwenza wake Mhes. Kalonzo Musyoka wangekuwa wameorodheshwa kama wagombezi nambari nane

kwenye orodha na hiyo ni nambari ya bahati kwani uchaguzi pia ungefanyika tarehe nane na ikifika tarehe tisa yeye angekuwa mshindi nambari moja, licha ya kuorodheshwa nambari nane ambayo ilikuwa ya mwisho. Anasema:

> Kura itapigwa tarehe 8, mwezi wa nane na Raila ni namba nane. Lakini ikifika tarehe tisa mwezi wa nane na Raila ni namba moja. Hio inaonyesha tumechukua hio *lane* ya nje. *Lane* ya nje, *the eighth lane* lakini kutoka mwisho tutakuwa namba moja.

Anatabiri ushindi ambao angeupata baada ya tarehe nane siku ya uchaguzi. Japo hakuupata huo ushindi, hii ni prolepsia ya nje kulingana na usimulizi wake. Tukio lingefanyika baada ya uchaguzi uliokuwa nje ya kipindi cha kampeni ambamo anasimulia matukio haya. Inajidhihirisha katika hotuba ya Ruto (2021) pia anapoahidi yale ambayo wangeyafanya baada ya kuchaguliwa. Anasema:

> Tumesema ajenda yetu, kipaumbele chetu ni kuhakikisha ya kwamba wakulima wengi wanaoteseka wapate mbegu, wapate mbolea, tuwatengenezee soko la mazao na tuhakikishe ya kwamba tumeondoa *mabroka* na wale *makartel* na wale *ma-monopoly* ndio wakulima wetu wapate haki yao wakiuza mazao yao na soko sawa sawa.

Hapa anadhihirisha ajenda yake na mojawapo wa yale ambayo anadhamiria kutimiza kupitia manifesto yake ambayo yangefanyika katika serikali yake atakapochaguliwa. Hayafanyiki katika simulizi yake lakini yanatarajiwa kufanyika baadaye. Imo katika hotuba yake Kenyatta (2017), anasema:

> Kabla ya serikali ya Jubilee, mfuko wa mbolea ulikuwa shilingi elfu mbili mia nane, leo hii mnanunua mbolea shilingi elfu moja mia nane na kutoka mwisho wa mwaka huu kwa sababu tumepanua *program* yetu ya mbolea, wananchi wa Kenya watakuwa wananunua mfuko wa mbolea shilingi elfu moja mia mbili.

Hii ni prolepsia nje, anaahidi yangefanyika mwishoni mwa mwaka ambayo hayafanyiki katika simulizi yake kipindi hicho.

#### 2.1.2.2 Prolepsia ya Ndani

Hii ni mbinu ya kubashiri yale ambayo yatafanyika kabla ya simulizi kukamilika. Inahusu matukio ya baadaye kurejelewa katika hadithi (hotuba) mapema na kufanyika wakati wake unapofika. Huwa ndani ya mipaka ya hadithi (Wamitila, 2008). Inaweza kuwa prolepsia tawasifu au prolepsia wasifu. Utafiti huu ulibainisha kuwa prolepsia ya ndani haijitokezi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

#### 2.1.2.3 Prolepsia Wasifu

Taarifa kuhusu matukio yanayotarajiwa kufanyika kuhusu mhusika mwingine au tukio jingine hutolewa katika wakati wa sasa wa hadithi. Matukio huhusu mhusika mwingine ambaye si yule anayerejelewa katika matukio ya sasa. Imejitokeza katika hotuba ya Kenyatta (2022) anapopigania uungwaji mkono wa rafikiye Mhes. Odinga kwa kueleza baadhi ya mambo ambayo yangefanyika katika serikali yake. Anasema:

> Hii itakuwa serikali ya kujumuisha wote, ya kujumuisha jamii zote za Kenya, ya kujumuisha wazee, akina mama na vijana haswa ndani ya serikali.

Dondoo hili linaonyesha jinsi serikali ya Odinga ingewaunganisha na kuwahusisha Wakenya wote katika uongozi wake. Tukio hili linasimuliwa kabla ya wakati wake kufika. Hii ni prolepsia wasifu.

Imejitokeza pia katika hotuba ya Odinga (2017) anapowaambia wafuasi wake kuwa baada ya uchaguzi, mpinzani wake Kenyatta angekuwa ametolewa mamlakani na kuwa raia wa kawaida.

Anasema:

> Uhuru, kazi yake itakuwa inakwisha siku ya Jumanne, Jumatano Uhuru atakuwa raia. Amri yake yote itakuwa haifanyi kazi.

Dondoo hili linaonyesha yale ambayo yangemfanyikia mhusika mwingine katika masimulizi ambayo hahusishwi nayo. Mhes. Odinga alikuwa anapiga kampeni za kujitafutia umaarufu na kuuza sera yake ndiposa akamrejelea mwenzake.

#### 2.1.2.4 Prolepsia Tawasifu

Hii ni aina ya prolepsia ambayo hutoa maelezo ya yale yatafanyika baadaye kuhusu mhusika au tukio linalorejelewa. Taarifa kuhusu matukio yanayosimuliwa au mhusika anayerejelewa katika wakati wa sasa wa hadithi hutolewa kuhusu kitakachofanyika kabla ya wakati wake kufika. Imejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Odinga (2017) anaahidi wafuasi wake kupambana na ufisadi iwapo angechukua nafasi ya uongozi. Anasema:

> Ufisadi umeenea, na mimi nitachukua huo ufagio wa ufisadi kutoka kwa Magufuli. Nitafagia nao ufisadi hapa Kenya na wote ambao ni wafisadi tutawapeleka nyumbani.

Mhusika huyu anatoa ahadi kuhusu kile ambacho angekifanya atakapopigiwa kura. Dondoo inarejelea suala la ufisadi ambalo huwa suala sugu katika kila kipindi cha uchaguzi. Anajirejelea yeye mwenyewe. Hii ni prolepsia tawasifu. Inajitokeza katika hotuba ya Ruto (2021) anapowaahidi wafuasi wake pale Nakuru kuhusu baadhi ya mambo atakayofanya katika serikali yake.

Anasema:

> Mimi nimefurahi sana kufika hapa Nakuru na mimi nataka niwaambie watu wa Nakuru hatutawaangusha. Tutahakikisha hii nchi itabaki imeungana na kile tulichokubaliana huku Nakuru kuwa taifa hili litaendelea kuwa na umoja na kuwa hakuna mali itakayoharibiwa wala maisha kupotezwa.

Hii ni prolepsia tawasifu kwa kuwa msimulizi anawaahidi wananchi amani na umoja; yale atakayofanya baadaye ikiwa atakuwa rais. Hatujui ikiwa alipata ushindi na kutimiza kile anachoahidi.

**2.2 Muda**

Wamitila (2002) anasema kuwa muda ni dhana inayorejelea uhusiano kati ya hadithi na swali iwapo tukio limechukua kipindi kirefu au kifupi? Kwa kuangalia muda anaochukua mtu kusoma hadithi fulani na muda wa matini, jambo ambalo ni gumu kwa kuwa wasomaji huwa na kasi tofauti na hotuba teule zilizorejelewa katika hadithi hii ni kauli zilizokuwa zinatolewa moja kwa moja. Ili kutatua hili, Rimmon-Kenan (2002) anapendekeza muda katika hadithi uangaliwe kwa wakati hadithi ambapo hadithi nzima huchukua na hupimwa kwa dakika, saa, wiki, miezi na wakati matini ambao ni wakati anaochukua mtu kusoma hadithi na hupimwa kwa kurasa au mistari. Muda hutumika kuonyesha uhusiano uliopo katika hadithi kiwakati. Hulenga kuonyesha uhusiano kati ya kipindi kinachochukuliwa na tukio kufanyika pamoja na kipindi kinachochukuliwa tukio kuwasilishwa.

Uhusiano kati ya wakati hadithi na wakati matini ni pale kasi ya usimulizi katika matini huchukua miundo miwili: kuharakishwa k.m tukio la muda mrefu kuwasilishwa kwa sentensi chache au dakika chache na kupunguzwa pale tukio la muda mfupi kuelezwa kwa sentensi au muda mwingi. Rimmon-Kenan (2002)

anabainisha vipengele vinne vya muda ambavyo ni udondoshi, mtuo, muhtasari na onyesho.

### 2.2.1 Udondoshi

Ni mbinu ambapo matukio fulani katika hadithi hayasimuliwi katika matini. Genette (1980) anasema kuwa hii ni kasi ya juu zaidi. Wakati matini huwa nunge au haupo ilhali wakati hadithi unaendelea. Msimulizi hulidondoa au kupuuza kusimulia jambo fulani iwapo si muhimu na kumpa msomaji au msikilizaji kujijazia mapengo yanayopatikana kiwakati. Ili kubainisha, huhitaji msikilizaji kumakinika wakati wa usimulizi wa hotuba teule (udondoshi batini) au ubainike moja kwa moja (udondoshi bayana).

#### 2.2.1.1 Udondoshi Bayana

Ni pale ambapo wakati matini huonyesha wazi kipindi cha muda ambacho kimerukwa au kuachwa nje katika simulizi. Msimulizi hueleza kiasi cha muda ambao umeachwa nje kabla ya tukio jingine analosimulia kujitokeza. Aina hii ya undondoshi imejitokeza kwa uchache katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hii ina maana ya kuwa ni wanasiasa wachache na huenda wakosekane wanaotumia mtindo huu katika harakati za kutafuta uungwaji mkono. Umejitokeza kwa uchache katika hotuba yake Kenyatta (2022) anaposema:

> Wengi hawakuwa wakiamini ya kwamba inawezekana baada ya miaka minne na nusu ya kwamba mimi na Raila tunaweza kuwa upande mmoja.

Dondoo hili linaonyesha udondoshi bayana kwa kutaja kipindi cha miaka minne, kauli yake haionyeshi nini kilichofanyika kwa muda wa miaka minne kilichokuwa kinawafanya watu wasiamini kuwa yeye na Raila wanaweza kuungana. Matukio yanayofanyika kati yao na kuwafanya wananchi wasidhani wanaweza kufanya kazi pamoja hayajatajwa. Imetumika na Odinga (2017) katika mkutano wake wa siasa anapowaalika wafuasi wake katika karamu ya ushindi wake ikulu. Anasema:

> Jumamosi wiki ijayo, tutafanya karamu kwenu kule katika ikulu. Nyinyi nyote mmealikwa kuja ikulu kwa karamu. Sawa sawa?

Kuna matukio ambayo yanafanyika kutoka siku hii anayowahutubia wafuasi wake hadi Jumamosi ya wiki ifuatayo anayowaalika wafuasi kwa karamu. Kipindi hiki kimejitokeza wazi lakini matukio yake hayajatolewa. Huu ni udondoshi bayana.

#### 2.2.1.2 Udondoshi Usio Wazi

Aina hii inaonyesha kuwa matukio fulani yameachwa nje na muda wake halisi ambamo yalitokea haujitokezi wazi. Hutumia kauli kama miaka/ siku nyingi/ kidogo/ chache baadaye na umedhihirika katika hotuba yake Ruto (2021) anaposema:

> Mimi nimekuja hapa Nakuru County mara nyingi. Nimekuja mambo ya barabara, nimekuja hapa mambo ya maji, nimekuja Nakuru mambo ya stima, nimekuja Nakuru mambo ya kanisa. Nimekuja Nakuru hii mambo mengi.

Mdokezo huu hauonyeshi ni kwa kipindi gani amezuru Gatuzi la Nakuru, anasema ni mara nyingi. Matukio yanayofanyika wakati huo ni machache tu ambayo ameyataja lakini mengi yaliyofanyika akizuru na kati ya kipindi kimoja hadi kingine cha ziara yake hayajasimuliwa.

#### 2.2.1.3 Udondoshi Batini

Mwananaratolojia Genette (1980:108) anasema udondoshi huu hujitokeza pale muda katika hadithi unakosa kutajwa. Hujitokeza msomaji anapogundua kuna pengo baina ya matukio yanayofuatana kiwakati. Kwa kiasi huashiria kuwepo kwa udondoshi usio wazi kwani muda hautajwi na hakuna maneno yatumiwayo kuudhihirisha. Umedhihirika katika hotuba yake Odinga (2022) anaposimulia mchuano wa mechi wa kuigiza shindano kati ya mrengo wa Azimio na Kenya kwanza anaposimulia refarii kuingia uwanja na anaposema Wetangula alikuwa anashukiwa kujaribu kumhonga refarii, anasema alionywa na bado kushika adabu. Anasema:

> Naona refarii anaingia kwa uwanja. Huyo Wetangula alishukiwa ati alikuwa anataka kuhonga refarii. Alionywa na inaonekana bado kushika adhabu.

Katika dondoo hili, muda umepita na mengi yamefanyika kabla ya refarii kuingia uwanjani. Matukio ya muda huo hayajasimuliwa; ni nani aliyesema Wetangula alitoa hongo, mbona alitaka kutoa hongo, alishikwa vipi, ni nani aliyemwonya na alimwonya vipi? Haya ni baadhi ya maswali ambayo msomaji atajiuliza kwani hayajarejelewa katika matini. Huu ni udondoshi batini.

#### 2.2.1.4 Udondoshi Dhahiri

Hapa muda katika hadithi hujitokeza wazi. Mpito wa kiwakati kati ya matukio hubainika. Waweza kuwa wazi au usio wazi. Umejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa kenya.

Kenyatta (2017) anasema:

> Wenzetu, kwa muda mchache sana wa miaka minne, tumeweza kuongeza idadi ya wakenya ambao tulipata wakiwa milioni mbili ambao walikuwa wameunganishwa kwa huduma ya stima.

Muda umedhihirishwa kuwa miaka minne ambapo wakenya wameunganishwa kwa stima. Hauko wazi, amesema tu wakati wote wa miaka minne. Msimulizi hajaeleza iwapo Wakenya wamekuwa wakiunganishwa kila mwaka katika miaka minne aliyotaja na iwapo tendo hilo lilikuwa linachukua mwaka mzima au la.

### 2.2.2 Mtuo

Huhusu maelezo anayoyatoa msimulizi ambayo yana au hayana uhusiano na hadithi katika hadithi yake. Huwa tofauti na yale maelezo yanayoendeleza mtiririko wa hadithi. Hudhihirisha kasi ya chini katika hadithi. Wamitila (2003) anaifafanua kama dhana inayoeleza jinsi ya kudhihirika kwa kasi – hadithi. Huweza kuwa maelezo kuhusu mandhari, mhusika, uzungumzi nafsia wa mhusika. Mtuo umejitokeza katika hotuba ya Odinga.Anasema haya:

> Tuko hapa na aliyekuwa rais wa Jamhuri ya Afrika Kusini – South Africa, Mhes. Thabo Mbeki yuko hapa, amekuja kushuhudia uchaguzi.

Maelezo kumhusu Thabo Mbeki ni ya ziada na hayahusiani na mtiririko wa matukio ya usimulizi wake. Anataja tu kuonyesha tu baadhi ya wageni au watu maarufu walioambatana naye katika mkutano huo wa kisiasa.

Katika hotuba yake Kenyatta, anasema:

> Lakini kuna wengine ambao wako na uwezo kushinda wale wengine, si ni kweli? Mmoja wao akiwa ndugu yangu Kalonzo Musyoka ambaye ameketi mbele yetu. Lakini ameweka tamaa yake chini kwa kulilia taifa la Kenya. Nataka tusimame na tumpigie makofi kwa ushujaa wake.

Hapa msimulizi anaacha usimulizi wake na kuanza kumsifu mhusika pamoja na kuwarai wafuasi wake wampigie makofi. Hii inadhihirisha mtuo katika masimulizi yake kwani alikuwa anamtafutia uungwaji mkono Mhes. Odinga.

### 2.2.3 Muhtasari

Katika muhtasari, kasi ya usimulizi huharakishwa kwa kutumia kauli zisizo ndefu au kwa kubana muda fulani. Wakati matini huwa fupi ikilinganishwa na wakati hadithi. Kisa kirefu kinachochukua muda mwingi katika masimulizi hufupishwa na kuelezwa kwa maneno machache. Rimmon-Kenan (1983: 104).

Muhtasari unajitokeza katika hotuba yake Odinga (2022) anapobuni na kusimulia mchuano wa mechi ya kandanda, anasema:

> Wameanza mpira, naona Mudaa na mpira, anaenda na mpira, anampatia Khalwale, Khalwale anaenda na mpira, anaenda na mpira Khalwale, amempatia Malala. Malala na mpira, na mpira Malala, Malala na mpira. Oooh ameteleza na kuanguka chini! Huyo mchezaji Malala ananonekana ameanguka chini, inaonekana ameumia kidogo, anabebwa kupelekwa nje lakini anarudi uwanjani mpira unaendelea sasa. Khalwale na mpira, anampatia Wetaa, Wetaa na mpira. Oparanya anakanyaga yeye, anamnyang'anya mpira. Lakini mpira unarudi tena kwa Kenya kwisha, wanaenda na mpira, wanaenda kwenye goli ya Azimio, mpira ndio huo unaenda kwa Bunyasi, anampatia Washiali, anamrushia Khalwale. Khalwale na mpira, anapiga shoot! Lakini golikipa Mama Elsie Muhanda anaudaka huo mpira bila wasiwasi wowote. Mpira unarudi, Mama Elsie anarusha mpira kule mbele kabisa, wanaazimio wanapata mpira. Pande ile ya Azimio na mpira, Tindi Mwale na mpira, anampatia Wangwe, Wangwe na mpira, anampatia Oparanya, Oparanya na mpira, Oparanya na mpira, anampatia Barasa, Barasa amemchenga, amemchenga tena, amechenga ya tatu, amempa yule

> kijana Mugabe. Mugabe na mpira, Mugabe na mpira, ndaaani, ndani, ndani, ndanii, *goaaal!*

Hapa muhtasari unajidhihirisha kwani mechi ya kandanda huchukua dakika tisini ilhali hapa matukio yote ya dakika hizo yamesimuliwa katika aya moja katika mechi hii ya kubuni. Unajitokeza pia katika hotuba yake Mhes. Ruto anaporejelea mswada wa BBI. Anasema:

> Kama kweli BBI ilikuwa ni ya kupeleka pesa kwa wananchi, tafadhali leteni mswada bunge wa *Finance Bill* wa kuongeza pesa kwa *counties*. Utapitishwa bunge na kaunti ya Nakuru zikiwemo zingine watapata pesa zao.

Kulingana na kanuni za Bunge la Kenya, mchakato wa kupitishwa mswada bunge hupitia hatua sita katika vikao tofauti vya bunge ambapo husomwa kwanza bila kujadiliwa, usomwe kwa mara ya pili na ujadiliwe, upelekwe kwenye vikao vya kamati na hatua nyinginezo ambapo hujadiliwa na mengi kufanyika kabla ya kukubaliwa. Mengi hayasimuliwi na msimulizi na ametumia maneno machache kuyaelezea katika kauli moja. Huu ni muhtasari.

### 2.2.4 Onyesho

Wamitila (2002) anasema kuwa hii ni njia ambayo huleta uigizaji katika matini yoyote ile. Naye Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa dayolojia ni mbinu bora ya kudhihirisha onyesho katika simulizi. Aidha, mazungumzo ambayo hayana mfumo wa kidayolojia hudhihirisha onyesho. Wahusika hujitokeza moja kwa moja wakizungumza na wengine katika dayolojia hivyo kudhihirisha usawa kati ya wakati hadithi na wakati matini.

Hotuba teule za wanasiasa wa Kenya zimesheheni onyesho. Katika mikutano yao ya kisiasa wahusika wanasemezana na wafuasi wao moja kwa moja. Kwa mfano Kenyatta (2022) anasema:

> Nataka kuona kwa mikono ni wangapi wamesema tumekubaliana ya kwamba tutaitembea hii safari tukiwa pamoja, si ni hivyo? *Are we together? We shall walk together?*

Maneno haya yanadhihirisha jinsi wanasiasa huwashirikisha wafuasi katika masimulizi kwa kuwauliza maswali ya kutaka kuwaunga mkono ambapo wafuasi hujibu kwa kuinua mikono au kutoa kauli za kukubaliana nao. Onyesho linajitokeza katika simulizi yake Ruto, anasema:

> Watu wa Nakuru, mnataka tubadilishe katiba ama mnataka tubadilishe uchumi kwanza?

Dondoo linadhihirisha maudhui ya uchumi na katiba baadhi ya mambo ambayo huuzwa katika sera za kisiasa. Anauliza hadhira yake swali hili ili kuonyesha suala ambalo angelishughulikia kwanza katika serikali yake kwa kuonyesha wapinzani wake hawamjali mwananchi kwanza.

### 2.3 Umara/ Idadi Marudio

Hiki ni kipengele kinachodhihirisha tukio limetokea mara ngapi na kusimuliwa mara ngapi katika matini. Tukio huenda likajitokeza mara moja katika hadithi lakini kurejelewa mara kadha katika matini. Tukio laweza kurudiwa katika sehemu tofauti za matini na huenda lisirudiwe jinsi lilivyo katika sehemu nyingine kutokana na utofauti wa muktadha.

Genette (1980) anaurejelea umara kama idadi marudio, anasema ni mahusiano kati ya simulizi na daijesia, tukio haliwezi kutendeka tu, bali linaweza tendeka tena na tena. Kauli hii inakubaliana naye Wamitila (2002: 144) anayesema umara ni mara ambazo matukio hurejelewa katika hadithi na mara za kusimuliwa. Anasema tukio huweza tendeka mara moja na kusimuliwa mara moja (usimulizi mosi), kusimuliwa mara kadhaa (usimulizi rudufu) na tukio linalofanyika mara kadhaa kusimuliwa mara moja (usimulizi banifu).

### 2.3.1 Usimulizi Mosi

Tukio katika hadithi hutokea mara moja na kurejelewa au kusimuliwa mara moja au wakati mmoja katika matini. Utafiti huu umebainisha kuwa kipengele hiki hakikutumiwa na wanasiasa katika hotuba zao teule kwani wao wana mazoea ya kurudia matukio na kauli ili kusisitiza ujumbe wao. Ule unajitokeza kama usimulizi mosi pale tukio linapotajwa mara moja, utafiti umeonyesha sio usimulizi mosi kwani yale yanayosimuliwa baadaye baada ya tukio huhusiana nalo, jambo linalofanya utafiti kukata kauli kuwa si usimulizi mosi.

### 2.3.2 Usimulizi Rudufu

Usimulizi huu huhusisha tukio kufanyika mara moja lakini kurejelewa mara kadha na msimulizi. Maneno yanayotumika yanaweza kubadilika kulingana na muktadha yanamopatikana lakini kinachorudiwa ni kile kile. Utafiti huu ulidhihirisha uwezo wa wanasiasa kukitumia kipengele hiki katika hotuba zao. Kwa mfano, katika hotuba ya Odinga (2017) katika Bustani la Uhuru anatoa shukrani kwa Wakenya kuhusiana na mambo kadhaa. Tendo hili la kuwashukuru mara nne kwa kuwataja kiumri, na kulingana na baadhi ya matendo katika miktadha tofauti ya yale anayotumia kuisuta serikali iliyokuwepo.

Anasema:

> Sasa siku ya leo nataka tu, kutoa shukrani kwa Wakenya wote kutoka pembe zote za Kenya. Tumeungana na Wakenya kule Mkoa wa Magharibi, Mkoa wa Nyanza, Bonde la Ufa, Nairobi, Mkoa wa Kati, Mashariki, Mashariki Kaskazini na Pwani na wote wamesema Raila na Kalonzo tosha. Natoa shukrani kwenu Wakenya kwa ile heshima ambayo mmetupa sisi na kuonyesha ya kwamba nyinyi mko tayari kwa mabadiliko. Nataka kutoa shukrani kwa vijana wa Kenya. *The youth of Kenya who have led the revolution, this is the youth revolution for change in our country and the change will come on the 8th, Tuesday next week.*

Baadaye anaendelea kuiuza sera yake, kukashifu suala la ukabila na kuwashukuru Wakenya tena. Anasema:

> Natoa shukrani kwa vijana wa Kenya kwa kujiepusha na siasa za ukabila.

Huu ni usimulizi rudufu kwani tendo la kuwashukuru Wakenya linafanyika mara moja lakini linarejelewa mara kadha kwa kuonyesha wale wanaopewa shukrani na kinachosababisha shukrani kutolewa kwao. Inajitokeza katika hotuba yake Ruto (2021) pia anapokashifu mswada wa BBI. Anasema:

> Nataka kuwaambia nyinyi watu wa Nakuru, BBI ulikuwa mpango wa ulaghai, mpango wa udanganyifu zaidi kuwahi kufanywa na utawala wowote.

Hapa swala la mswada wa BBI lilifanyika mara moja kabla ya kusimamishwa na mahakama. Analirejelea katika hotuba yake, kisha anaendelea kuuza sera kwa kuonyesha mabaya yake kabla ya kuirudia kauli hii tena.

Anasema:

> BBI ulikuwa mpango wenye udanganyifu zaidi kuwahi kufanywa na watu. *How do you dare* kutuambia kuwa mnataka kuwa na rais wa kifalme mwenye mamlaka ya kuhujumu bunge kupitia uteuzi?

### 2.3.3 Usimulizi Banifu

Hujitokeza pale ambapo tukio linalojitokeza mara kadha wa kadha katika hadithi linasimuliwa mara moja katika matini. Katika hotuba yake ya kisiasa anayotoa hapo Nakuru, Ruto (2021) anasema kuwa amezuru kaunti hiyo mara nyingi kwa shughuli tofauti tofauti, ila katika usimulizi wake tukio hili limesimuliwa mara moja katika matini licha ya kuwa katika hadithi amezuru huko siku tofauti na mara nyingi. Anasema:

> Mimi nimekuja hapa Nakuru *County* mara nyingi. Nimekuja hapa mambo ya Barabara, nimekuja mambo ya maji, nimekuja Nakuru mambo ya stima, nimekuja Nakuru mambo ya kanisa. Nimekuja Nakuru hii mambo nyingi.

Tendo lake kuenda Nakuru linafanyika siku tofauti na kwa madhumuni tofauti kulingana na kauli yake. Yote haya yanasimuliwa mara moja hivyo kudhihirisha kuwepo kwa usimulizi banifu katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza kipengele cha wakaa na kuonyesha jinsi kinavyodhihirika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti umeonyesha kuwa kipengele hiki ni muhimu katika simulizi, hotuba ikiwa mojawapo kwa sababu matukio yote yanayohutubiwa hutokea kiwakati. Utafiti umeonyesha jinsi matukio yamepangwa ki-anakroni (kipengele cha mpangilio) kwa matumizi ya analepsia na prolepsia. Muda

kama kipengele cha wakaa umejitokeza, mtindo wa udondoshi umejitokeza kwa wingi ikilinganishwa na onyesho, muhtasari na mtuo, vipengele ambavyo pia vimejitokeza. Idadi ya utokeaji wa matukio imebainika, kuna yale yaliyotokea mara moja na kusimuliwa mara moja na mengine mara nyingi. Utafiti umebainisha yaliyotokea mara nyingi na kusimuliwa mara moja japo miundo ya sentensi na maneno iliyotumika katika urudiaji sio sawa kutokana na tofauti za kimuktadha. Kipengele hiki kimedhihirika kuwa cha muhimu katika kazi yoyote ya kinathari na kimesaidia kuelewa vyema ujumbe, wahusika na maudhui katika hotuba teule.

# SURA YA TATU

# USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA HOTUBA TEULE

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia wahusika na kuonyesha njia mbali mbali ambamo wahusika wamesawiriwa. Utafiti umeanza kwa kutoa ufafanuzi wa dhana ya wahusika pamoja na kuonyesha mbinu tofauti zitumikazo kuwasawiri wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

## 3.1 Wahusika

Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua dhana wahusika kwa kueleza kuwa ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa katika mazingira ya kitamaduni, kijiografia, kihistoria au kijamii ambayo huwa ya msanii. Naye Wamitila (2003) anasema kuwa mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya fasihi anayafanana na binadamu kwa kiasi fulani kitabia, kiitikadi, kifalsafa na kimaadili. Sifa hizi hutambulishwa na usemi wake, matendo yake na kauli za wengine kumhusu. Anaendelea na kuainisha aina za wahusika kuwa mhusika mkuu anayerejelewa kote katika kazi ya sanaa na anatumika kuendeleza dhamira ya msanii, mhusika msaidizi ambaye huathiriana na mhusika mkuu kuendeleza dhamira ya mtunzi, mhusika bapa ambaye habadiliki kitabia wala kisifa kutoka mwanzo hadi mwisho wa simulizi na mhusika duara anayebadilika kitabia katika simulizi.

Senkoro (2011) naye anasema kuwa wahusika ni watu au viumbe ambao hunuiwa kuwakilisha tabia, dhana na mawazo ya watu katika tungo za kifasihi. Wamitila (2008) anasema kuwa wahusika ni dira muhimu katika kazi za kifasihi kwa kuwa watendaji wakuu wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi zenyewe. Wao ndio ambao huendeleza msuko au matukio, maudhui na dhamira

ya msanii, yaani wao ni msingi wa kazi yoyote ile ya kinathari, mojawapo ikiwa ni hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

Rimmon-Kenan (2008) naye anaeleza kuwa wahusika ni watu au viumbe wanaoonekana katika tukio au maandishi ya kisanaa na huwa na jukumu la kutoa maana katika hadithi. Ni wale wanaoshiriki katika matukio ya kifasihi na huwa na mabadiliko au maendeleo, matendo na tabia zao. Anasema kuwa wao husaidia kuunda miundo ya kihistoria, kihisia na kuchangia kueleza jumla ya mandhari na ujumbe wa kazi hiyo.

Wahusika ni kipengele muhimu cha fani. Wao huwekwa katika mandhari yanayomsaidia kuwasilisha hoja zake kutokana na matendo, maingiliano na fikra zao. Wanaweza kuwa wanyama, mizimu au binadamu wanaoumbwa kuwasilisha ujumbe. Kwa ujumla, wahusika ni viumbe wa kisanaa ambao hubuniwa na msanii katika mazingira mahususi ya kisanii na hutumiwa kama njia ya kufikisha ujumbe au maadili katika hadhira.

### 3.2 Usawiri wa Wahusika

Dhana ya usawiri wa wahusika imefafanuliwa na wasomi tofauti. Wamitila (2008) anasema kuwa wasomaji na wahakiki wa fasihi hutegemea sifa kadha kuwaelewa wahusika. Hii ni kutokana na maumbile yao, tabia zao, lugha zao uhusiano wao na wahusika wengine, hisia zao wenyewe, mazingira na mandhari yao, kiwango chao cha elimu na kadhalika. Huu ni usawiri.

Ponera (2014) anafafunua usawiri wa wahusika kama kitendo cha kuwachora, kuwatambulisha, kuwafafanua na kuwakuza wahusika kwa kuwapa usemi, matendo

na uwezo unaofanana nao. Anaendeleza kwa kusema kuwa majina wanayopewa pamoja na lugha wanayotumia kifasihi hujumuisha dhana ya usawiri. Mawazo yake yanawiana na yale ya BAKIZA (2010) jinsi wanavyofafanua neno "sawiri." Kwa hivyo, usawiri wa wahusika ni jinsi ya kuwajenga wahusika, kuwapa majina, matendo na sifa kwa misingi ya dhamira na maudhui ya msanii katika tungo za kisanaa za kifasihi.

### 3.3 Mbinu za Kuwasawiri Wahusika

Rimmon-Kenan (1983) anaeleza kuwa wahusika wanaweza kusawiriwa kwa njia mbili kuu ambazo ni njia ya moja kwa moja ambapo sifa za mhusika huelezwa kwa vivumishi vya sifa na njia isiyo ya moja kwa moja ambapo mhusika husawiriwa kutokana na maelezo ya mhusika mwingine, au maelezo ya msimulizi (Keen, 2003).

#### 3.3.1 Usawiri wa Moja kwa moja/ Bainishi

Hii ni mbinu ya kusawiri wahusika ambapo msanii hutumia vivumishi hasa vya sifa, nomino dhahania na aina nyingine ya maneno kueleza kumhusu mhusika. Sifa ambazo ni za kuaminika hutajwa moja kwa moja kumhusu. Sauti ya msimulizi huwa na nguvu katika matini husika na anapotaja sifa za mhusika, kauli yake huchukuliwa kwa uzito mwingi ikilinganishwa na pale zinapotajwa na mhusika mwenzake. Katika mbinu hii, msimulizi hutoa wasifu wa mhusika moja kwa moja.

Wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya wamesawiriwa kwa njia ya moja kwa moja kutokana na kauli na matendo yao. Kwa kutumia mbinu hii, wanasiasa hupata nafasi ya kuonyesha mawazo yao ya chuki au mapenzi yao kwa wahusika fulani ambao ni wanasiasa wenzao. Wanaitumia ili wafuasi wao waweze kuwaelewa wapinzani wao kwa mtazamo wao badala ya kungoja wao wawaelewe kutokana na

matendo ya wahusika hao binafsi. Aidha, kulingana na Chomsky (1988:01) wanaitumia kwa nia ya kuendeleza propaganda kwa kutowapa nafasi kutathmini tabia wenyewe.

Katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya, wahusika wamesawiriwa kwa njia ya moja kwa moja jambo ambalo utafiti huu umetolea mifano. Katika hotuba ya Odinga (2017), anayoitoa katika Bustani la Uhuru anaeleza kwa kusema kuwa mpinzani wake Mhes. Kenyatta ni mnafiki na mjeuri, anasema:

> Asante, asante Wakenya wezangu, nimeona kama mmechoka na Uhuru, mimi Raila Amolo Odinga nimechoka na unafiki wa Uhuru Kenyatta, nimechoka na ujeuri wa Uhuru Kenyatta, sasa leo namwambia Uhuru Kenyatta na Ruto yake, aje na timu yake. Mimi niko na timu yangu ya NASA tukutane nao uwanjani ana kwa ana.

Maelezo yake msimulizi kuhusu Kenyatta ni ya moja kwa moja kwani anaieleza hadhira yake kuhusu sifa zake Kenyatta kwa kutumia kivumishi “nafiki” na “jeuri.” Sauti yake msimulizi na kauli yake ni ya kuaminika kwa wafuasi ambao wako tayari kumuunga mkono katika kiti cha urais. Japo kauli yake inaweza kuwa ya kutoaminika kuhusu mpinzani wake, wafuasi hawana nafasi ya kubaini ukweli na kwa kuwa wako tayari kumuunga mkono, kauli zake kuhusu mpinzani wake ni za kuaminika. Utafiti huu umeonyesha jinsi wahusika wanavyosawiriwa na msimulizi ili kubainisha chuki yake dhidi ya mpinzani wake. Anaendelea kudhihirisha sifa za mpinzani wake kwa kusema:

> Tukiongea hapa, yale ambayo yameibwa tangu Jubilee waingie kwa serikali ni shilingi bilioni mia tatu hamsini, pesa ya raia ambayo wameiba. Ufisadi umeenea.

Katika dondoo hii, anaisuta serikali iliyomo mamlakani kwa kutaja jinsi ufujaji wa pesa za umma unavyofanyika. Anabainisha sifa zake Mhes. Kenyatta na serikali yake kuwa fisadi. Kauli zake msimulizi kama kiongozi wa upinzani ni za kuaminika. Anadokeza sifa hasi za wahusika ambao ni wapinzani wake ili kupata uungwaji mkono na wananchi ili kuiondoa serikali iliyopo mamlakani na achukue hatamu za uongozi. Utafiti umedhihirisha jinsi wanasiasa huwasawiri wahusika ambao ni wapinzani wao kwa kutumia sifa hasi.

Usawiri wa moja kwa moja pia unajitokeza katika hotuba ya Mhes. Kenyatta (2022) pale KICC anapotueleza kumhusu Mhes. Kalonzo Musyoka ambaye alikuwa tayari ameiacha nia yake ya kugombea urais na kumuunga mkono Mhes. Odinga aliyekuwa akizinduliwa kama kinara wa Azimio la Umoja. Maelezo anayoyatoa msimulizi kumhusu Musyoka kujitoa katika kinyang'anyiro hicho na kuwa tayari kulipigania taifa na Odinga yanamdokeza kama mwananchi mzalendo. Anasema:

> Hakuna kiongozi ambaye hana uwezo wa kutafuta kiti cha urais wa nchi ya Kenya. Wote wako na huo uwezo na wengi wameweka tamaa ama *ambition* zao kando kwa sababu wanataka kuona Kenya ikishikana na haswa kwa sababu vile nimesema hakuna mmoja wetu ambaye hana uwezo lakini kuna wengine ambao wako na uwezo kushinda wale wengine, si ni kweli? Mmoja wao akiwa ndugu yangu Kalonzo Musyoka ambaye ameketi mbele yetu. Lakini ameweka tamaa yake chini kwa kulilia taifa la Kenya. Nataka tusimame na tumpigie makofi kwa sababu ya ushujaa wake.

Maelezo anayotoa msimulizi katika dondoo hili kumhusu mhusika Mhes. Musyoka yananuia kumsawiri kama mzalendo na shujaa kutokana na tendo lake la kuacha azma yake ya kugombea urais na kumwachia mwenzake Mhes. Odinga. Miller (1995) katika chapisho lake *On Nationality* anasema uzalendo sio tu mapenzi kwa taifa bali ni wajibu wa mwananchi kuchangia kwa maslahi na kudumisha maadili ya taifa lake.

Dondoo hili linaonyesha yeye ni mzalendo kwani yuko tayari kuacha chochote mradi taifa lake liweze kuendelea. Aidha tendo lake la kuwachia mwenzake nafasi kwa kuwa ni mwenye uwezo zaidi ni tendo la kishujaa. Huu ni usawiri wa moja kwa moja kwani msimulizi anatoa maelezo ya moja kwa moja kumhusu; matendo yake na sifa zake.

Usawiri wa wahusika kwa mbinu ya moja kwa moja umeweza kubainika katika kauli ya Mhes. Ruto (2021) katika hotuba anayoitoa hapo Nakuru. Anasema:

> Na wakati mlikuwa na kiburi, mkatuambia *nobody can stop reggae*, ndio mjue kuna mungu Kenya hii, hio *reggae* ilisimama ndio muwache kiburi na madharau.

Katika dondoo hili, msimulizi ameweza kutoa maoni yake kulingana na alivyowafahamu wapinzani wake. Katika dondoo anawaonyesha kama wenye kiburi na madharau. Hii ni kutokana na harakati za wapinzani wake kuendeleza na kuupitisha mswada wa BBI kwa kutozingatia maoni ya Wakenya wa kawaida na kutofuata kanuni za kikatiba. Keltner na wenzake (2003) katika utafiti wao *Power, Approach and Inhibition* wanasema kuwa watu walio katika nafasi za mamlaka na utawala ikiwemo wanasiasa hudhihirisha kiburi na kukosa hisia za huruma. Hii inabainika katika kauli ya msimulizi. Walitumia mamlaka na nguvu walizokuwa nazo katika serikali kuupitisha kwa haraka kwa kutouhusisha mrengo wake. Jambo hili linamfanya awasawiri kama wenye kiburi na madharau, kauli yake inabainisha usawiri wa wahusika wa moja kwa moja katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Aidha, anaendelea kuusawiri mchakato wa BBI kama wenye udanganyifu.

Anasema:

> BBI ilikuwa njama ya udanganyifu mkubwa zaidi kuwahi kufanywa na watu wowote. Mnawezaje kuthubutu kutuambia kwamba mnataka rais wa kifalme mwenye mamlaka ya kuhujumu bunge kupitia uteuzi, na mwenye mamlaka ya kuhujumu mahakama kupitia kwa *Ombudsman?*
>
> (tafsiri yangu)

Kutokana na hisia za msimulizi (anayetoa hotuba) anaeleza kutopendezwa na mswada wa BBI. Anatoa maelezo mafupi kuuhusu yanayomfanya kuusawiri moja kwa moja kwa kuupa sifa hasi. Anatumia mbinu hii kuwafanya wafuasi wake kumwamini na kuwavutia katika mrengo wake.

Usawiri wa wahusika moja kwa moja huiwezesha hadhira kumtambua mhusika ikikutana naye sehemu yoyote ile katika matini au katika mandhari mengine kwani huwawezesha kufahamu sifa zao, na sio rahisi sifa hizo zisahaulike moja kwa moja. Utafiti umedhihirisha wanasiasa hutumia usawiri wa moja kwa moja wa wahusika kwa kuwapa sifa hasi ili kuonyesha ubaya na chuki dhidi ya wapinzani wao na kuwapa sifa chanya ili kuwasifia wenzao kuungwa mkono na wapigaji kura. Aidha wanafanya hivyo kwa kuwa wanajua wapigaji kura wengi hupuuza tendo la kujitathminia wenyewe tabia walizonazo wanasiasa (wahusika) wanaorejelewa. Aidha, wengine huwa wamefumbwa na kasumba ya kuwaamini viongozi wao na kufuatilia chochote kile kinachosemwa. Wakati wa usimulizi, mbinu hii hukosa kuipa hadhira nafasi ya kutathmini ukweli na tabia alizonazo mhusika.

### 3.3.2 Usawiri Usio wa Moja kwa Moja (Usawiri Timbe)

Katika mbinu hii, tabia za mhusika hazitajwi moja kwa moja bali hudhihirishwa kwa kupitia matendo, usemi au kauli zake, mwonekano wa nje, majina ya majazi anayopewa, mazingira anamopatikana mhusika na mavazi anayoyavalia. Rimmon -

Kenan (1983) anasema kuwa njia hii ya kumsawiri mhusika humwongoza msomaji au hadhira (msikilizaji) kubaini sifa za mhusika kwa kuchunguza mwonekano wake. Naye Keen (2003) anasema kuwa mbinu ya kumsawiri mhusika kwa njia isiyo ya moja kwa moja huhusu maelezo ya wahusika wengine kumhusu ambayo humwezesha msomaji kumwelewa. Utafiti huu uliangazia usawiri wa wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kuijadili kupitia vijimada vifuatavyo:

a) Mazingira
b) Usemi
c) Muonekano wa Nje
d) Analojia
e) Matendo

**3.3.2.1 Mazingira**

Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa maeneo aliyomo mhusika (chumba, nyumba, barabara, mji), mazingira ya kijamaa (familia, tabaka) na hata mazingira ya kikazi hutumika kumsawiri mhusika. Utafiti huu umeonyesha uwezo wa wanasiasa kuweza kuwasawiri wahusika kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kuyarejelea mazingira wanamopatikana. Kwa mfano, katika hotuba ya Ruto (2021), anayerejelea mazingira ya Nakuru wanamoanzia siasa zao na Mhes. Kenyatta yanatusaidia kumfahamu zaidi. Anasema:

> Mimi ninawauliza watu wa Nakuru, mko tayari tuendelee na *project* tulianza apa Nakuru ya amani ya Kenya? Mko tayari tuendelee na mradi wa umoja tulianza hapa Nakuru? Mko tayari tuendelee na mkataba tulieka hapa Nakuru ya kwamba Kenya haitapiganwa tena? Mali haitaharibika tena kutoka wakati huo, mkataba wa hapa Nakuru tuendelee nao?

Kauli katika dondoo hili inatolewa na Mhes. Ruto akiwa Nakuru, anaonyesha kuwa anakumbuka ahadi walizowatolea wafuasi wao awali hapo Nakuru, yuko tayari kuzitimiza na kuwa mrengo wake wa kisiasa ni ule wa kueneza amani nchini. Anapowaeleza kuwa yuko tayari kutimiza yale waliyoahidi, msimulizi anajisawiri kwa kudhihirisha sifa ya mpenda amani, kuyarejelea yale waliyonena mwaka 2017 wakiwa Nakuru utafiti umeweza kudhihirisha kuwa yeye ni mwenye kumbukumbu nzuri na mwaminifu kwani anayakumbuka aliyoyasema na yuko tayari kuyatimiza.

Katika hotuba ya Kenyatta (2017), anaeleza kuhusu mazingira wanamoishi wanasiasa na kuwasawiri kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Anasema:

> Msikubali kupiganishwa vijana. Hawa viongozi ambao wanawapiganisha, watoto wao wanaishi manyumba kubwa kubwa Nairobi. Nyinyi ndio mtakaoumia jameni. Wewe mpende mwenzako, Jirani yako, yule mnaishi naye kama ndugu yako. Tusikubali tupigane wenzangu.

Dondoo hili linatoa maelezo kuhusu kule wanakoishi wanasiasa ambao huwachochea vijana kusababisha vita ilhali wao na watoto wao huishi kwenye makao salama katika mitaa ya kifahari ambako vita na fujo haziwezi kuwafikia kutokana na usalama wanaoupata katika mitaa hii. Msimulizi anawasawiri wahusika hawa kuwa wanafiki. Kamusi ya Karne ya 21 (2014) inaeleza kuwa mnafiki ni mtu anayefanya mambo kinyume na anavyoahidi. Kwa hivyo, tendo la wao kuchochea vijana ili kusababisha vita ilhali wao wanaishi sehemu salama ambako hawataathirika ni unafiki, kwani hawatadhurika na vita hivyo. Aidha, wao kuishi majumba makubwa jijini kwenye usalama wa kutosha kumemwezesha mtafiti kuwasawiri kama fisadi. Rose-Ackerman (2016) anaeleza kuwa mhusika fisadi ni mtu anayepata kitu kwa kutumia uwezo alionao kwa manufaa yake binafsi. Wanasiasa wanajinufaisha kutokana na siasa za

uchochezi na umaarufu walionao kwa wafuasi wao kusababisha vita ili wao wajinufaishe kwa kupata uongozi na vile vile mali kutokana na nafasi za uongozi wanaoupata kutokana na umwagaji damu. Aidha, dondoo hili limebainisha mazingira ya utabaka. Wanasiasa wanaowachochea vijana wanaishi majumba makubwa jijini Nairobi. Kauli hii ya msimulizi imemwezesha mtafiti kuwasawiri wanasiasa kama wa tabaka la juu kinyume na wale wanaochochewa ambao huenda ni wa tabaka la chini na wanakoishi hakuna usalama.

#### 3.3.2.2 Usemi

Mhusika husawiriwa kwa mbinu isiyo ya moja kwa moja kutokana na mazungumzo yake au fikira za akilini mwake. Kamusi ya Karne 21 (2014) inaeleza kuwa usemi ni maneno yanayosemwa kwa maana maalum. Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa mhusika anaweza kusawiriwa kupitia usemi anaoutoa au mawazo yanayompitikia akilini. Kile mhusika anachosema kumhusu mhusika mwingine kinaweza kutumika kubainisha sifa zake au sifa za mhusika anayemrejelea. Anaendelea kusema kuwa umbo la usemi ni njia ya uhusika kwenye matini, lugha ya mhusika huweza kutofautishwa na ya msimulizi. Umbo huonyesha asili ya mhusika, mandhari anamoishi au tabaka lake.

Utafiti huu umerejelea usawiri wa wahusika usio wa moja kwa moja kwa kuonyesha kuwa wanasiasa teule wanawasawiri wahusika na kusawiriwa na mtafiti kupitia usemi kwa kurejelea mambo mawili ambayo ni:

a) Jinsi wanavyozungumza.
b) Mazungumzo yao kujihusu au kuwahusu wahusika wengine.

#### 3.3.2.2.1 Jinsi anavyozungumza mhusika

Kutokana na jinsi anavyozungumza mhusika, wasifu wake hujulikana. Aidha, anaweza kuwa na lafudhi au kauli fulani zinazomtambulisha. Katika hotuba ya Odinga (2017) jinsi anavyowaongelesha wafuasi wake kwa kauli za kuwasisimua kunadhihirisha yeye ni mcheshi. Anasema:

> Hayaa! Vijana hoyee! Nairobi hoyee! Leo wale ambao walikuwa na tashwishi watajua kuna *Tsunami*, nilisema *Tsunami* itakuja. Imeanza leo, kuelekea tarehe nane, nane, nane, nane. Ni nane mara tatu.

Katika dondoo hili, utafiti umebainisha mhusika Odinga kuwa mwenye sifa ya ucheshi. Imebainika kwamba mara nyingi yeye huanza usemi wake kwa kutumia neno "haiyaaaa" usemi ambao humtambulisha. Wasifu unaojitokeza na kuonyesha kuwa ni mtu anayependa kutumia kauli "hayaaa." Huku kumebainisha kuwepo kwa usawiri wa wahusika kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kurejelea usemi wa mhusika hususan kwa kurejelea jinsi mhusika anavyozungumza.

Usemi umetumika kumsawiri Ruto kama mcha mungu. Katika hotuba yake anayoitoa hapo Nakuru 2021, anasema:

> Na msijaribu kulaumu mtu kwa mambo ya BBI, mungu ndiye aliyesimamisha mambo ya BBI. Ilikuwa imepitishwa kwa kaunti, ilikuwa imepitishwa kwa *senate*, ilikuwa imepitishwa kwa bunge. Mungu ndiye aliyesimamisha huko kwa mahakama. *So* wacheni, mnalalamikia nani?

Katika dondoo hili, msimulizi anaamini yale yaliyofanyikia mswada wa BBI yalifanyika kwa sababu Mungu hakuruhusu ukubaliwe kinyume na matarajio ya

wapinzani wake. Kauli hii imefanya utafiti kumsawiri kama mcha mungu kutokana na usemi wake kwa kumtaja mungu na kuamini yanayofanyika ni kutokana naye. Umejitokeza katika hotuba ya Kenyatta (2017) ambapo utafiti huu unamsawiri kama mpenda amani. Anasema:

> Na tukasema wakati huo 2013, tukasema tushinde au tushindwe, sisi haja yetu ni ya amani ya Wakenya waishi pamoja.

Usemi huu unadhihirisha msimulizi ni mpenda amani. Aidha, yeye kusema kuwa washinde au washindwe haja yao ni kuhakikisha Kenya kuna amani kumefanya utafiti huu kumsawiri kama mzalendo. Hajali iwapo atashinda au kushindwa mradi kuwe na amani. Hii ni kwa sababu eneo la Nakuru liliathirika sana katika vita baada ya uchaguzi wa 2007 washiriki walipopigania ushindi (Mohammed, 2010). Yeye hayuko tayari kukubali tukio kama hilo lifanyike tena, huku ni kupenda taifa lake na huu ni uzalendo.

#### 3.3.2.2.2 Mazungumzo Kujihusu au Kuwahusu Wahusika Wengine

Mhusika anaweza kusawiriwa kulingana na yale anayoyasema kujihusu (wasifu wake) au yale anayoyasema kuhusu wahusika wengine.

##### 3.3.2.2.2.1 Mhusika na Wasifu wake

Haya ni yale ambayo mhusika anasema kujihusu. Utafiti huu umebainisha kuwa wanasiasa hutumia maneno ya kujisifu au kauli kujihusisha na yale mambo ambayo wafuasi wao wanapitia, ili kujihusisha na hali yao ya maisha na kupata uungwaji mkono. Mtindo huu umejitokeza katika hotuba ya Kenyatta.

Anasema:

> Wenzetu, kwa muda huu wa miaka minne, pole pole kila mwaka tumekuwa tukiongeza pesa ya elimu, pesa ya *capitation*. Tukaongeza ya *primary* na *secondary*. Tukaenda tukahakikisha ya kwamba mashule yetu yote yako na stima. Tukatoka hapo, tukasema ya kwamba watoto wetu hawatakuwa wanalipa kufanya mitihani. Mwaka huu, tumeanza kutumia shilingi bilioni kumi na kupanua shule zetu za upili, ndio mwaka ujao kila mtoto wa Kenya aweze asome kutoka *Standard one* mpaka *Form 4* bila malipo tena. Tunaelewana wenzangu?

Kupitia usemi huu, utafiti umeweza kumsawiri mnenaji kama mpenda maendeleo. Anayataja yale maendeleo ambayo serikali yake imefanya. Halikadhalika, anaonyesha jinsi anavyoyajali maslahi ya wananchi kwa kuwarahisishia mambo kama vile kuongezea mgao wa pesa kwa sekta ya elimu ili wasilipe karo. Mtindo huu umejitokeza pia katika usemi wa Ruto (2021), anasema:

> Sisi tuko upande mwingine tunataka kubadilisha Uchumi. Watu wa Nakuru, mnataka tubadilishe Katiba ama mnataka kubadilisha Uchumi kwanza?

Katika dondoo hili, usemi wake msimulizi umefanya utafiti kumsawiri kama mwanamapinduzi. Anapanga kubadili mfumo wa kiuchumi kutoka uliokuwepo wa *Trickle down* hadi mfumo mpya wa *Bottom up* ambapo wanaoangaziwa ni wananchi wa tabaka la chini. Wanaangaziwa kusaidiwa kwa kupewa pato la juu ili kuwawezesha kupata pato la kuweza kuiendeleza serikali ya kitaifa.

#### 3.3.2.2.2.2 Mhusika na Wasifu wa Mhusika Mwingine

Kauli anazotoa mhusika kuhusu mhusika mwingine hutumiwa kumsawiri mhusika anayerejelewa. Mbinu hii imejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Odinga (2017) anasema:

> Wakenya wamelia kila mahali, gharama ya maisha imepanda, unga *revolution*, ungaa, ungaaa. Wakenya wamelia kuhusu mambo ya ukosefu wa ajira. Hakuna kazi kwa vijana, ufisadi umezidi Kenya yetu.

Usemi huu wake Odinga unawasawiri wananchi wa Kenya kama wenye majuto na malalamishi. Wanajuta na kulalamika kuhusiana na kupanda kwa gharama ya maisha hasa bei ya unga. Wanajuta kuchagua uongozi ambao ufisadi umezidi. Inajitokeza pia katika hotuba ya Ruto (2021), anasema:

> Jambo la pilli, mimi nataka nikubaliane na nyinyi vile tutaenda mbele, wale ambao tunashindana nao wanatuambia ati ya muhimu ati *priority* kwa Kenya ni vile tutaongezea rais mamlaka, ni vile tutatengeneza vyeo vya wadosi, ni vile tutaunda mpango wa kugawana mamlaka. Sisi katika jeshi ya *Hustler Nation* tunasema *priority* yetu ni kutafutia vijana wetu ambao hawana kazi, ajira kwanza.

Kauli hii yake kuhusu wapinzani wake kuwa na mipango ya kuwanufaisha wao wenyewe badala ya kuyajali masuala yanayomwathiri mwananchi wa kawaida kwanza yamefanya utafiti huu kuwasawiri wapinzani wake kama wenye ubinafsi. Usemi wake unaonyesha kuwa wao wanajijali na kujipangia mema kwanza badala ya mwananchi kwanza.

#### 3.3.2.3 Muonekano wa Nje

Katika mbinu hii, sifa za mhusika huelezwa kwa kurejelea maumbile yake, mitindo yake ya mavazi na nywele. Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa kuna uhusiano wa

moja kwa moja wa jinsi mhusika anavyoonekana kwenye uso na sifa zake za kipekee. Mbinu hii hujadiliwa katika mada ndogo zifuatazo:

a) Maumbile
b) Mavazi

Utafiti huu umebainisha kuwa mbinu hii haijatumika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hii ni kwa sababu hakuna usimulizi wowote ambao umetumiwa na wanasiasa rejelewa ambao unaangazia maumbile na mitindo ya mavazi au nywele. Japo sampuli iliyorejelewa ni ile ya video za *Youtube* ambapo kuna picha za maumbile na mavazi (utafiti haukuwasawiri wahusika kwa kuangazia haya), usimulizi ulijikita kwenye matini – yale yanayosemwa na wanasiasa hawa katika hotuba zao.

### 3.3.2.4 Analojia

Kamusi ya Karne ya 21 (2014) inasema kuwa analojia ni mchakato wa kulinganisha vitu viwili au hali mbili kwa madhumuni ya kuthibitisha kuwa zinafanana. Tabia ya kitu kufuata mkondo au sura ya kitu kingine kilichotangulia. Kwa hivyo, analojia ni neno ambalo huelezea ulinganishi wa vitu ambavyo vinahusiana kwa namna mbali mbali. Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa analojia huchukuliwa kama kijalizo cha uhusika wala sio mbinu ya kipekee ya kuwasawiri wahusika. Hii ni kwa sababu uwezo wa analojia kuwasawiri wahusika hutegemea ufahamu wa kimbele kwa namna nyingine kwa misingi ya sifa ambazo uwezo huo umekitwa. Mbinu hii hufananisha kwa kutumia majazi, istiari na ulinganishaji wa wahusika.

#### 3.3.2.4.1 Majazi

Hii ni mbinu ya kuwapa wahusika majina kulingana na tabia au wasifu wao. Wamitila (2003:106-7) anasema kuwa majina hutumika kuelekeza sifa za wahusika kimuonekano, kiakustika, kimatamshi na kimofolojia. Rimmon-Kenan (1983)

akiwanukuu Hamon (1972) na Ewen (1980) anasema, kulingana na Hamon (1972) majina yanaweza kufanana na sifa za mhusika kwa namna jina linavyoonekana, linavyosikika, linavyotamkwa na umbo lake. Naye Ewen (1980) anaeleza kuwa kuna uhusiano wa kisemantiki baina ya jina na tabia ya mhusika.

Mbinu hii imetumiwa na wanasiasa katika hotuba teule. Imebainika kuwa wanawapa wanasiasa wapinzani wao majina ya majazi ili kuwasawiri kwa kuwapa sifa hasi, kuwakashifu na kulenga kutaka wafuasi wao kuwaambaa na kuwaunga mkono.

Kwa mfano, katika hotuba ya Kenyatta (2017), ametumia majazi kumsawiri mpinzani wake Mhes. Odinga. Anasema:

> Tuliongea na wenzetu wa *African Development Bank*, wakatupatia pesa ya kujenga hapa Mwache *Dam*, Itaare *Dam*. Tukaenda tukaanza kazi. Bw. Kitendawili, *Thirty-two billion* ya kuleta maji ya kutosha Nakuru *town*, Rongai na sehemu ya Kuresoi. Watu wawe na maji ya kutosha. Mwenzangu Bw. Kitendawili akasema ya kwamba ati tukichukua hio maji tutakausha mto na maji hayatafika *L. Victoria*.

Dondoo hili linaonyesha jina analopewa Mhes. Odinga ambalo ni Bw. Kitendawili. Jina hili ni la majazi linaloafikiana na tabia ya Odinga. Hii ni kutokana na tabia yake ya kupenda kutega na kutegua vitendawili kwa kuwashirikisha wafuasi wake katika mikutano ya kisiasa. Mbinu hii imejitokeza katika simulizi ya Odinga (2022) anaposimulia mchuano wa kandanda kati ya Azimio la Umoja dhidi ya Kenya Kwanza. Anasema:

> Joho anamchenga, amemchenga Arap Mashamba. Ndio huyo ameanguka chini. Arap Mashamba ameanguka chini. Inaonekana kama ameumia, inaonekana ni kama alikuwa amebeba vitu vingine pale. Inaonekana ni kama alikuwa amebeba pesa, anaanguka nayo chini.

Msimulizi hapa amempa mhusika jina la majazi “Arap Mashamba.” Kwa kiasi jina hili linasawiri tabia yake Mhes. Ruto. Hii ni kutokana na yeye kutuhumiwa katika kesi kadha zilizomhusisha na unyakuzi wa ardhi ya umma na ya watu binafsi.

#### 3.3.2.4.2 Ulinganuzi wa Wahusika

Katika mbinu hii, wahusika wawili huwekwa katika muktadha sawa. Usawa au utofauti katika tabia zao ndizo zinazoshadidia sifa zao. Mbinu hii ya ulinganishi hujulikana kama kulinganisha kwa kinyume. Mtindo huu umejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Katika hotuba ya Odinga (2017) analinganisha serikali ya Kenyatta (Jubilee) na ile ya rais wa Tanzania Magufuli. Ulinganisho wake unamsawiri Kenyatta kama fisadi ilhali Magufuli kuwa mwadilifu, kinyume chake. Anasema haya kwa kulinganisha gharama ya mradi wa reli ya SGR kule Tanzania na hapa Kenya. Anadhihirisha kuwa reli ya Tanzania ni ndefu na imegharimu pesa chahe ikilinganishwa na reli ya Kenya ambayo ni fupi na imegharimu pesa nyingi. Anasema:

> Hata reli Wanatanzania wanajenga sasa SGR kutoka Dar es Salaam kupitia Dodoma kuingia Tabora kuelekea Mwanga halafu ipite mpaka Bujumbura na iende mpaka Kampala. Hii yenu itakwama hapa hapa Naivasha kwa sababu ya ufisadi.

### 3.3.2.5 Matendo

Mbinu hii inaeleza kuwa tabia za mhusika hutambulika kutokana mambo anayoyafanya mara moja au kila mara. Ingawa tendo la mara moja halionyeshi sifa bainifu za mhusika, haimaanishi kuwa sifa zinazotolewa sio za mhusika. Tendo la mazoea huibua vipengele vya mhusika visivyobadilika. Matendo haya huwekwa katika kategoria:

#### 3.3.2.5.1 Tendo la Utekelezaji

Matendo ya mhusika humsaidia msomaji kung'amua sifa za mhusika. Mhusika asipofanya jambo msomaji hawezi kutambua tabia zake. Hii imejitokeza katika hotuba za wanasiasa. Kwa mfano, katika hotuba ya Odinga mwaka 2022 kule Kakamega na mwaka 2019 kule Kibra, anasimulia mechi ya kuigiza kati ya timu yake (chama chake – Azimio la Umoja) na timu ya wapinzani wake. Kuna hotuba nyinginezo ambapo pia anasimulia mechi ya kandanda. Tabia hii yake ya kusimulia mechi za kandanda imefanya utafiti huu kumsawiri kama mpenzi wa michezo ya kandanda.

#### 3.3.2.5.1 Tendo la Kunuia

Mbinu hii hurejelea tendo la mhusika ambalo halijatekelezwa lakini kinatarajiwa kufanywa. Hili huwa tendo ambalo wahusika wengine hawajaligundua. Mtindo huu haujajitokeza katika hotuba yoyote ya wanasiasa teule.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii imejadili wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti umedhihirisha uwezo wa wanasiasa wa Kenya kuwasawiri wahusika kwa mbinu za usawiri wa moja kwa moja na usawiri usio wa moja kwa moja kwa kutolea mifano. Mbinu hizi zimewezesha kueleweka kwa sifa za wahusika waliokuwemo katika simulizi za hotuba teule.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI USEMI DHIMA ZAKE, ZA WAKAA NA WAHUSIKA

## 4.0 Utangulizi

Sehemu hii imechunguza jinsi lugha au usemi unavyowasilishwa na wahusika katika simulizi kutokana na mawazo yanayowapitikia akilini. Usemi ambao umejadiliwa hapa ni ule ambao huelezwa kwa njia ya maelezo ya msimulizi. Aidha, sehemu hii imejadili dhima za vipengele vya Naratolojia vya usimulizi ambavyo ni wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi.

## 4.1 Uwasilishaji Usemi

TUKI (2019) wanasema kuwa usemi ni namna au jinsi ya kusema. Kwaka (2018) katika utafiti wake "Uhakiki wa wakati na uwasilishaji usemi kama vipengee vya Usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa*" anasema kuwa katika kazi yoyote ya fasihi, lugha ni kipengee muhimu, huhusishwa na wahusika wanaotumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo, usemi ni ujumbe unaojitokeza katika matini.

Uwasilishaji usemi ni njia ambazo msimulizi hutumia ili kutoa ujumbe kwa hadhira lengwa. Muiya (2022) anasema kuwa mbinu ambazo hutumika kuwasilisha usemi wa wahusika ni sawia na zitumikazo kuwasilisha mawazo yao. Wamitila (2008:96) anasema kuwa jinsi lugha inavyowasilishwa katika kazi ya fasihi ni suala muhimu sana katika kazi ya uchanganuzi wa fasihi. Anaendelea kufafanua usemi kama tamko ambalo lina msemaji na msemewa na huhusisha mbinu mbalimbali za matamko kama sehemu ya shughuli za kijamii. Mwananaratolojia Rimmon-Kenan (2002) akinukuu chapisho lake Plato, *Republic* (1963: 638), anasema kuwa Socrates anaainisha mbinu mbili za kuwasilisha usemi ambazo ni daijesia ambayo ni njia ya maelezo ya msimulizi ambapo matukio yanaelezwa au kusimuliwa jinsi yalivyotokea na mimesia

ambapo lugha au usemi wa wahusika unawasilishwa kwa njia iliyo wazi. Wahusika wanajibizana na kuakisi hali halisi kama ilivyo katika drama au tamthilia.

Leech na Short (1981) wanasema kuwa mtindo unaotumika kuwasilisha usemi wa wahusika ndiyo unaotumika kuwasilisha fikira zao wazo linaloshahibiana na Plato. Wanadai kuwa mbinu hizi zikitumika huibua mifumo mingine ya usemi na fikira kama vile usemi halisi huru, fikira halisi huru na fikira taarifa huru. Katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya, utafiti huu umebainisha kuwa ujumbe huwasilishwa kwa njia ya usemi halisi ambapo ujumbe huwasilishwa moja kwa moja jinsi ulivyosemwa na mhusika, usemi taarifa ambapo ripoti ya ujumbe uliosemwa na mhusika hutolewa bila kuzingatia muundo wake asilia, usemi halisi huru unaohusisha uzungumzi nafsi wa mhusika na usemi taarifa huru. Kila mbinu ya uwasilishaji usemi imejadiliwa katika utafiti huu.

### 4.1.1 Usemi Halisi

Mwananaratolojia Prince (1987: 43) anasema kuwa usemi halisi ni aina ya diskosi ambayo matamshi au fikira za mhusika hutolewa au kunukuliwa jinsi zilivyowasilishwa. Naye Wamitila (2008: 97) anaeleza kuwa usemi halisi ni uwasilishaji wa maneno yaliyotamkwa na msemaji kama alivyoyatamka kwa alama za mtajo. Manfred (1995:N3.2.1) anasema kuwa ni maneno yanayosemwa na mhusika katika simulizi na huweza kunukuliwa moja kwa moja kama yalivyotamkwa. Kwa hivyo, usemi halisi ni maneno halisi yanayotolewa na mhusika na hunukuliwa na msimulizi kwa alama za mtajo na maneno kama vile “akasema” na “akawaambia.” Aidha, usemi halisi hudhihirishwa kwa kutumia viambishi viwakilishi vya nafsi ya kwanza katika maongezi ambavyo ni **ni** (umoja) na **tu** (wingi), vivumishi vimilikishi

**_angu** (umoja) na **_etu** (wingi), viashiria vya karibu hapa, huku na humu na vielezi vinavyoonyesha wakati uliopo.

Utafiti huu umebainisha kuwa uwasilishaji usemi katika hotuba teule zote umetumia usemi halisi. Hii inajitokeza zaidi katika kauli zao wasimulizi ambao pia ni wahusika, ambao mara kwa mara wanatoa ahadi zao kwa kutumia nafsi ya kwanza. Ni wazi kuwa hotuba zote hutolewa katika usemi halisi. Katika hotuba ya Odinga (2017) usemi halisi unajitokeza anapotumia kitenzi chenye kiambishi cha nafsi ya kwanza "**ni**" na kitenzi kiarifu "wakasema" anasema:

> Ninatoa shukrani kwa vijana wa Kenya kwa kujiepusha na siasa za ukabila. Mara hii mtaona kama kura itatoka pembe zote za Kenya. Hapa mkoa wa kati. Hapa hapa vijana wengi wamejitokeza wakasema "*Central* for Raila."

Dondoo hili limetumia kitenzi kiarifu "wakasema" anapoyanukuu moja kwa moja maneno yaliyosemwa na vijana. Aidha ametumia kiambishi cha nafsi "ni" kudhihirisha wazi huu ni usemi halisi. Imejitokeza katika hotuba ya Ruto (2021) anapotumia nafsi huru "mimi" anasema:

> Mimi ninataka niwashukuru sana. Mimi nimefurahi kufika hapa Nakuru. Na mimi ninataka niwaambie tutatembea hii safari pamoja. Na mimi ninataka niwaeleze nikimalizia wale walituletea *reggae* na hio mambo ingine, sisi tutakuwa na mpango.

Maneno "mimi," kiambishi cha nafsi "tu" na "hapa" ni kauli zinazotumika katika usemi halisi kulingana na Ngowe (2017) Hii ni ithibati tosha ya usemi wa wanasiasa katika hotuba teule umewasilishwa katika usemi halisi. Neno "mimi" aidha linaonyesha ukaribu uliopo kati ya mzungumzaji na wale wanaozungumziwa, yaani

mwanasiasa na hadhira yake. Mtindo huu unadhihirika wazi katika hotuba ya Kenyatta (2017), anasema:

> Tuko hapa siku ya leo, tukiwa sasa kwa kipindi cha lala salama. Huu ndio mkutano wetu wa mwisho wa *campaign* zetu. Na sisi tuliamua ya kwamba mkutano wetu wa mwisho tunataka kuenda *capital city* ya siasa za Kenya, na ni hapa Nakuru. Ndio tufungie siasa zetu hapa Nakuru.

Katika dondoo hili, Kenyatta ambaye ni msimulizi na mhusika katika simulizi hii anadhihirisha kuwa hotuba huwasilishwa katika usemi halisi. Anatumia maneno "siku ya leo," "tuko" na "mkutano wetu," kauli hizi ni fikira za mhusika mwenyewe na zinajitokeza moja kwa moja jinsi zinavyotoka mawazoni mwake, hii ni kulingana na Mwananaratolojia Prince (1987) Usemi halisi umejitokeza pia wahusika wanapotumia vitenzi viashiria kama vile "anasema," kwa mfano, Kenyatta (2017) anaendelea kusema:

> Mwezangu ambaye twashindana naye akasimama akasema, "Angalia hawa watu ati wanapatia stima, wanawaekea nyumba ya nyasi stima!" Huyo ndio mtu wa kitendawili, na akasema kwa mkutano wa hadhara.

### 4.1.2 Usemi Taarifa

Short (1991) anasema kuwa katika mbinu hii ya kuwasilisha usemi, maneno hayatolewi moja kwa moja kama yalivyosemwa na msemaji. Badala yake yanaripotiwa na msimulizi wa nafsi ya tatu. Manfred (2005: 67) anasema kuwa katika mbinu hii msimulizi huonyesha kilichosemwa na mtu mwingine na matokeo ni kuwa baadhi ya maneno huweza kubadilika. Naye Wamitila (2008:102-103) anasema kuwa katika usemi halisi msimulizi hunena kilichosemwa na mhusika mwingine kwa

kutumia maneno yake binafsi bila kutumia alama za mtajo au vishazi viarifu. Anasema:

> Usemi wa taarifa hauna matumizi ya alama za nukuu na huwepo maneno yanayoonyesha kuwepo kwa usemi wa taarifa. Aidha huwa na maneno kama vile “kwamba.” Matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza na pili “mimi” na “wewe” huchukuliwa na viwakilishi vya nafsi ya tatu, “yeye.” Pia viwakilishi vya mahali na wakati hubadilika na pia pana mabadiliko kuhusiana na mwelekeo wa vitenzi kutoka “kuelekea hadi” mbali na.

Kwa hivyo, usemi taarifa ni ripoti ya kile kilichosemwa na mtu mwingine kwa kutotilia maanani mbinu au muundo asili wa kilichosemwa. Viwakilishi vya nafsi ya tatu hutumika. Uwasilishaji huu huenda na usimulizi wa nafsi ya tatu ambao huangazia masimulizi kwa mtazamo wa nje.

Utafiti huu umedhihirisha usemi huu katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Imebainika kuwepo kwa usimulizi wa nafsi ya tatu kwani wasimulizi walirejelea yale yaliyosemwa na wahusika wengine. Kwa mfano, Ruto (2021) anasema:

> Saa hizi wanatuambia kwamba kuna *counties* zimekosa pesa kwa sababu ya BBI.

Anaendelea kwa kusema:

> Saa zingine wanatuambia ati walipoteza *constituency* hii, walipoteza *constituency* ile.

Katika madondoo haya, msimulizi anarejelea yale yaliyosemwa na wapinzani wake wakati mswada wa BBI ulipuziliwa mbali mahakamani na waasisi wake kuanza kueleza wafuasi wao baadhi ya mambo ambayo waliyapoteza kutokana na uamuzi wa mahakama. Usemi taarifa unajitokeza kutokana na vitenzi viarifu kama vile

“wanatuambia kwamba” aidha wakati uliopita “li” unarejelewa kuonyesha kuwa kauli ilisemwa kitambo. Jinsi anavyoeleza Wamitila (2008) anayesema kuwa nyakati hubadilika na kuwa wakati uliopita wakati kauli iliyosemwa na msemaji halisi inasemwa na msemaji aliye katika nafsi ya tatu. Usemi taarifa unajitokeza pia katika hotuba ya Odinga (2017) anasema:

> Hapa mkoa wa kati kati. Hapa hapa, vijana wengi wamejitokeza wakasema *Central for Raila*. Wameshasema milioni moja, kura watanipigia. Kutoka Mkoa wa *Central* hapa.

Katika kauli hii, msimulizi anarejelea yale yaliyosemwa na vijana ambao ni wafuasi wake katika Mkoa wa Kati. Anadai kuwa walikuwa wamemwahidi kumuunga mkono. Sehemu hii ilikuwa ngome ya wapinzani wake, Ipsos (2017) kwa hivyo anayesema haya yaliyosemwa na vijana kuonyesha ana umaarufu kinyume na yaliyosemwa na shirika la kuchukua maoni la Ipsos Kenya. Usemi taarifa umebainika katika dondoo hili kutokana na kitenzi kiarifu “wameshasema,” “wakasema” na kiambishi cha nafsi ya tatu “wa” kimetumika katika kitenzi “watanipigia.” Haya yote hutumika katika usemi wa taarifa, tendo hili linakubaliana na maelezo ya Manfred (2005: 67). Uwasilishaji huu pia unajitokeza hotuba ya Kenyatta (2022) anapomuunga mkono Odinga katika Kongamano la Azimio la Umoja. Anamsifu Mhesh. Musyoka kwa kuacha nia yake ya kuwania urais na kumuunga Mhesh. Odinga. Anamsifu na kuyasema maneno yaliyosemwa na Mhesh. Musyoka wakati huo. Anasema:

> Kwanza kabisa, ningependa tumshukuru Mhesh. Stephen Kalonzo Musyoka kwa sababu sio ya kwamba hangeweza, anaweza. Lakini akasema hatakuwa mmoja wa wale wa kugawanya Wakenya, anataka tutembee pamoja. Tumshukuru Mhesh. Stephen Kalonzo Musyoka.

Msimulizi katika dondoo hili anadhihirisha matumizi ya usemi wa taarifa. Anayarejelea yale yanayosemwa na Mhesh. Musyoka kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu “a” na vitenzi viashiria “akasema,” na “anataka.” Maneno haya yamefanya utafiti huu kukubaliana naye Wamitila (keshatajwa) jinsi alivyonukuliwa tayari hapa kubainisha kuwepo kwa uwasilishaji wa usemi kwa kutumia usemi taarifa.

### 4.1.3 Usemi Halisi Huru

Usemi halisi huru unasawiana na usemi halisi, tofauti ni kuwa katika usemi halisi maneno ya msemaji hunukuliwa na kishazi kiarifu hutumika ilhali katika usemi halisi huru, mojawapo wa sifa hizi (kunukuliwa au kishazi kiarifu kutumiwa) huondolewa. Wamitila (2008: 99) anaonyesha haya anaposema:

> Usemi halisi huru hutokea pale ambapo vishikizi vya kauli ya msemaji (maneno yanayofuata dondoo au nukuu) na alama za kunukuu za kuonyesha kuwa huo ni usemi halisi zimeondolewa.

Kwa mujibu wa Collier (1992) hii ni aina ya usemi halisi ambapo kishazi tangulizi hakitumiki katika unenaji ingawa alama za mtajo huwa zimedumishwa. Anasema, kishazi tangulizi kikitolewa katika usemi wa wahusika, dayolojia kati ya wahusika huharakishwa. Hivyo kupunguza muda wa kuisimulia hadithi. Usimulizi wa aina hii huweza kuzua utata wa kuelewa ni nani anayesema nini kati ya wahusika tofauti iwapo kishazi tangulizi hakipo, kumwacha msomaji ajiamulie msemaji ambaye huenda asiwe sahihi hivyo kupotosha ujumbe uliokusudiwa. Haya ni kulingana na Barry (1995).

Naye Short (1991) anasema kuwa usemi wa aina hii hutokea katika sentensi ambazo huonyesha kuwa vitendo vya unenaji vimeshafanyika ingawa msimulizi

hajishughulishi na kutoa maana ya kilichosemwa. Wahusika huzungumza kwa zamu bila kuonyesha ni nani anayezungumza.

Katika mtindo huu wa uwasilishaji usemi, mhusika huwasiliana na hadhira yake moja kwa moja bila msimulizi kuingilia kati jinsi inavyofanyika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Licha ya hayo, uwasilishaji huu haujajitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hii ni kwa sababu yule anayetoa hotuba tayari anajulikana na kuonekana kwa hadhira yake kulingana na data ya video za *Youtube* iliyorejelewa. Aidha, mhusika anayetawala mazungumzo hapa ni anayesimulia kutoka mwanzo hadi mwisho.

Utafiti huu umebainisha kuwa mtindo huu wa kuwasilisha usemi huenda ukaleta utata kulingana na sampuli ya data iliyorejelewa. Usemi wa mhusika mkuu; anayehutubia unawasilishwa bila kishazi kiarifu jinsi mtindo huu unavyoelezwa na Wamitila (keshatajwa) na kupinga yale yanayosemwa na Barry (keshatajwa) kuwa msomaji huhitajika kujiamulia ni nani anayesema kinyume na kuwa katika hotuba tayari anajulikana. Isitoshe, hakuna mhusika mwingine anayezungumza naye kwa zamu kuonyesha jinsi vishazi viarifu vinavyodondolewa.

### 4.1.4 Usemi Taarifa Huru

Wamitila (2008) anasema kuwa usemi taarifa huru ni zao la kufanyia mabadiliko usemi wa taarifa kwa kuondoa baadhi ya maneno yanayoashiria usemi wa taarifa na kuyawakilisha na yale ya usemi halisi. Hapa, viambishi vya wakati, vibainishi na vielezi vya mahali vinavyohusishwa na usemi taarifa huwa vimeondolewa.

Wamitila (2008) wanaafikiana na Short (1991) wanapoeleza kuwa muundo wa usemi taarifa huru huchukua sifa zinazofungamana na usemi halisi. Hubainika kutokana na

mwingiliano baina ya matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya tatu, wakati uliopita na nafsi ya kwanza inayohusisha wakati uliopo.

Mwananaratolojia Rimmon-Kenan (2002) anasema kuwa usemi taarifa huru huwa na sifa za mabadiliko ya viwakilishi ambavyo huwa katika usemi halisi: nafsi ya kwanza na nafsi ya pili ambavyo hubadilika kuwa nafsi ya tatu katika usemi taarifa na usemi taarifa huru. Huondoa vitenzi na viunganishi. Viashiria vya mahali vya karibu havibadilishwi, vishazi vinavyoonyesha aliyesema maneno huondolewa.
Utafiti huu umebainisha uwasilishaji wa usemi kupitia usemi taarifa huru haujitokezi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hii ni kwa sababu utafiti umebainisha kuwa wanasiasa ambao ni wahusika wakuu na wasimulizi katika hotuba, hutoa kauli zao nyingi katika usemi halisi.

## 4.2 Dhima za Vipengele vya Wakaa, Wahusika na Uwasilishaji Usemi katika Hotuba Teule za Wanasiasa wa Kenya

Kamusi ya TUKI (2019) wanasema kuwa dhima ni neno linalorejelea wajibu mkubwa pamoja na uwezo wa kufanya jambo. Kwa hivo, dhima ni majukumu yanayotekelezwa na kitu fulani. Yaweza kuwa matumizi yake au umuhimu wa kitu kile. Utafiti huu umeonyesha umuhimu wa vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti umebainisha dhima za vipengele hivi ni kujenga maudhui na kuendeleza fani. Haya yamejadiliwa katika mada ndogo hizi:

### 4.2.1 Kujenga Maudhui

Njogu na Chimerah (1999: 21) wanasema kuwa maudhui ni jumla ya mawazo mapana yanayowasilishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelea. Wanaendelea

kusema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya maudhui na mtindo. Wanasema kuwa mtindo unaotumiwa kuwasilisha fasihi humwezesha msanii kuwasilisha maudhui yake. Utafiti huu umeangalia jinsi wanasiasa wanavyotumia mtindo wa usimulizi hasa vipengele vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi vinavyotumiwa kuwasilisha ujumbe.

Kulingana na Wamitila (2003: 189) na Mohamed (1995: 11) wanasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi ambayo huzuka katika uendelezaji na ukuaji wa dhamira ya kazi hiyo. Maelezo haya yanaafikiana na utafiti huu kuwa ni mambo ambayo msimulizi (mwanasiasa- ambaye ni mtunzi katika hotuba teule) huyarejelea kama lengo lake kuu la kutimiza anapopewa nafasi ya uongozi. Wanaafikiana naye Mbatiah (2011) anayeeleza kuwa maudhui ni jumla ya maswala yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi.

Maudhui ni ujumbe wa jumla unaojitokeza katika kazi ya fasihi. Hushirikishwa moja kwa moja na kuwasilisha dhamira katika kazi ya fasihi. Utafiti huu umebainisha kuwa wanasiasa wa Kenya waliweza kutumia vipengele vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi kukashifu baadhi ya mambo yanayofanyika ambayo wanayapinga na yale ambayo wanaahidi kuwa wangeyafanya wakipata uongozi. Huu ni ujumbe wa jumla (maudhui) unaojitokeza katika maongezi yao.

Stanzel (1984: 21-28) anaeleza kwamba msimulizi hutambulisha maudhui katika kazi ya kisanaa kwa kuwasilisha usemi wa mhusika, fikra zake, matendo na mihemko yake. Maelezo yake yamewezesha utafiti huu kubainisha uwezo wa kipengele cha uwasilishaji usemi kujenga maudhui. Hii ni kwa sababu jinsi mhusika anavyosimulia

hisia zake, kuwasilisha ujumbe wake na ujumbe na matendo ya mhusika mwingine, maudhui huibuka.

Naye Griffith (2010) anasema kuwa maudhui huwakilishwa kupitia vipengele mbalimbali vya kisanaa wakiwemo wahusika. Wahusika hutumiwa na mtunzi kama vyombo vya kuwasilisha ujumbe. Wahusika ni mojawapo wa kipengele cha usimulizi ambacho utafiti huu umebainisha usawiri wao katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya katika sura ya tatu. Matendo na usemi wao humwezesha msomaji kupata maudhui anayolenga kuyawasilisha mtunzi.

Utafiti huu umejadili kwa ujumla maudhui yanayotolewa na vipengele hivi kwani kila kipengele kinayadhihirisha. Kuyajadili maudhui katika kila kipengele kibinafsi kungesababisha urudiaji mwingi katika utafiti huu, maudhui yaliyobainika ni:

#### 4.2.1.1 Kuendeleza siasa

Hotuba zote zilizorejelewa katika utafiti huu zinahusiana na masuala ya kisiasa, zinatolewa na wanasiasa wakati wa kampeni wanapotafuta uungwaji mkono ili wachaguliwe kama rais.

Adero (2005: ix) anasema kuwa siasa ni dhana inayotumiwa kuelezea mfumo wa uendeshaji wa masuala ya kijamii katika taifa. Hujihusisha na maoni tofauti kuhusiana na maswala ya kidini, kiuchumi, kielimu, kabila na kitamaduni. Nao TUKI (2019) wanasema kuwa siasa ni itikadi inayofuatwa na kundi fulani la jamii ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo. Swala hili linabainika katika hotuba teule.

Ruto (2021) anasema:

> Mimi ninataka nikubaliane na nyinyi ya kwamba tutachagua MCA wa UDA ambaye anaelewa maana ya amani, ambaye anaelewa maana ya *Bottom Up,* ambaye ataanza kushughulikia mambo ya watu wadogo, mtatupatia wabunge wa bunge la hapa Nakuru ambao watashirikiana na sisi tuendeshe mambo ya *Bottom Up*? Mtatupatia wabunge wa UDA? Ambao watasaidiana nasi, kusukuma mambo ya *Bottom Up*?

Mwanasiasa huyu anapiga kampeni kwa kuwataka wananchi wa Nakuru kumuunga na kufuata msingi wake wa kuendeleza Uchumi wa taifa wa *Bottom Up* ambao ungekuwa unamjali mwananchi wa hadhi ya chini kiuchumi kwanza na wafanyibiashara wadogo (Citizen, 2022). Msingi huu unashikiliwa na chama chake cha UDA. Usemi wake unadhihirisha maudhui ya siasa kwani anapigania urais na kupata wafuasi katika mfumo wake wa Uchumi anaotaka kuendeleza jinsi wanavyoeleza TUKI (2019). Anarejelea siasa bado katika hotuba yake ya 2019. Anasema:

> Ile siasa ya zamani ya ugomvi na chuki na fitina na mambo ya ukabila, tumesema hio siasa haina nafasi katika Kenya ya karne ya ishirini na moja.

Kenyatta (2017) anadhihirisha siasa pia kwa kuwarai wananchi wampigie kura ya hatamu ya pili kama rais, anasema:

> Nawaomba, kwa heshima kubwa, kubwa sana, tarehe nane wiki ijayo mkubali, mjitokeze kwa wingi. Mzee wa kitendawili aende nyumbani saa mbili asubuhi awe ameenda nyumbani. Nakuru, mtatuunga mkono? Tutaendelea na kazi? Kazi itaendelea? Ebu nionyesheni kwa mikono nione ni wangapi wanasema kazi iendelee?

Jumla ya hotuba zilizorejelewa katika utafiti huu ni za kisiasa. Vipengele vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi vimesaidia kuyabainisha wazi maudhui haya.

#### 4.2.1.2 Kukashifu ufisadi

Rose- Ackerman (2006) anasema kuwa ufisadi ni matumizi ya nafasi aliyo nayo mtu ili kupata kitu au raslimali ya umma kwa manufaa binafsi. Nayo Kamusi ya Karne ya 21 (2014) inasema kuwa ufisadi ni utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali, tabia ya ubadhirifu. Wanaendelea kusema kuwa ni utoaji na upokeaji wa hongo. Ufisadi unaweza husisha kupokea kitu kwa kutozingatia maadili. Yaani, ufujaji au ubadhirifu au matumizi mabaya ya mali ya umma. Utafiti huu ulibaini kuwa, ufisadi ni swala kuu katika hotuba za kisiasa. Nia ya wanasiasa waliorejelewa ilikuwa ni kupambana na janga la ufisadi iwapo wangechaguliwa kama marais. Kwa mfano, Odinga (2017) anasema:

> Tukiongea hapa, yale ambayo yameibwa tangu Jubilee waingie kwa serikali ni shilingi bilioni mia tatu hamsini. Pesa ya raia ambayo wameiba. Ufisadi umeenea. Na mimi nitachukua huo ufagio wa ufisadi kwa Magufuli. Nitafagia nao ufisadi hapa Kenya, na wote ambao ni wafisadi tutawapeleka nyumbani.

Kauli yake inaashiria kuwepo matumizi mabaya ya pesa za umma katika serikali iliyokuwepo wakati huo ya Jubilee. Anasema kuwa takribani shilingi bilioni mia tatu hamsini ziliibiwa kutoka serikalini tangu wapinzani wake wauchukue uongozi. Anawaahidi wafuasi wake kupambana na ufisadi kwa kutumia mbinu na mikakati ya aliyekuwa rais wa Tanzania Mhes. Magufuli. Analitumia swala hili ili kuwavutia wafuasi ili kuweza kuchaguliwa kama kiongozi.

Ruto (2021) anasema:

> Mlikuwa na kiburi na mkatuambia hakuna yeyote atakayesimamisha *reggae*. Ndio mjue kuna Mungu Kenya hii, hio *reggae* ilisimama. Ndio mwache kiburi na madharau. Sijui kama tunaelewana rafiki zangu. Ndio mwache kiburi na madharau, ndio hio BBI imekwama na itakwama na itapotea, sijui kama tunaelewana?

Kauli yake inadhihirisha ufisadi. Anaonyesha jinsi serikali iliyokuwepo na upinzani walivyotumia uwezo na mamlaka kupitisha mswada wa BBI. Matumizi mabaya ya mamlaka kwa manufaa ya kibinafsi ni ufisadi, jambo linalotendeka kulingana na kauli yake mnenaji. Naye Kenyatta (2022) akimtawaza Odinga kama kiongozi wa Azimio la Umoja, anarejelea suala la ufisadi na kusema:

> Taifa letu la Kenya litasonga mbele na umoja. Taifa letu la Kenya litasonga mbele na kupigana na ufisadi. Taifa la Kenya litaendelea kuwa nchi ambayo itaheshimika kati ya nchi za dunia.

Hapa anadhihirisha kuwepo kwa ufisadi katika serikali na miongoni mwa Wakenya. Anawahakikishia wafuasi wake kwamba Odinga ndiye ana uwezo wa kulitatua janga hili hivyo kuwaomba wamuunge mkono.

#### 4.2.1.3 Kukuza uchumi

Kulingana na Kamusi ya Karne 21 (2014) Uchumi ni jumla ya mapato na matumizi ya watu katika nchi. Waweza kuwa pia taaluma ya mapato na matumizi ya nchi au watu. Suala la Uchumi ni kigezo kikubwa katika siasa na kila mwanasiasa hupigania kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa taifa lolote lile. Haya yote yanajitokeza wazi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

Kwa mfano, Ruto (2021) anapigania kuboresha Uchumi kwa kuanzisha mfumo mpya wa *Bottom Up*, anasema:

> Nawauliza watu wa Nakuru, tumesema tunaanza pale chini, ndio tunasema ni *Bottom Up*, kuanzia na wale hawana kazi, wale biashara yao ni kidogo, wale wanahangaika. Wakulima, tuanze nao, kila mtu tuwapandishe ngazi ya maendeleo. Biashara yao ipande ngazi hiyo. Watu wa Nakuru tunakubaliana ajenda ya UDA ikuwe hio? Ama mnasemaje watu wa Nakuru?

Kauli hii inathibithisha kuwepo maudhui ya Uchumi. Msemaji anaonyesha nia yake ya kubadili Uchumi wa taifa kwa kuuboresha iwapo atapewa nafasi ya kuliongoza taifa la Kenya. Anapanga kuubadili kwa kubadilisha mfumo na kuleta ule unaowajali wananchi wenye kiwango cha chini maishani. Obondo, Okello na Nandwa (2017) wanajadili kuhusu Uchumi na kusema kuwa mfumo mbaya wa uchumi ni chanzo cha maisha duni nao mfumo thabiti hupunguza uzito wa hali ya maisha. Uchumi unarejelewa na Kenyatta (2022) anasema:

> Na mimi sina shaka ya kwamba ana uwezo, ana nia na mwenyezi mungu atamjalia aweze kuhakikisha ya kwamba taifa letu la Kenya linasonga mbele na maendeleo.

Maudhui ya Uchumi yanajitokeza wazi katika kauli hii. Ili taifa liweze kukua kimaendeleo, Uchumi wa taifa hilo unafaa kuboreshwa. Maudhui haya yanajitokeza kwa wingi pia katika hotuba yake aliyoitoa mwaka wa 2017 anapoorodhesha baadhi ya mafanikio ambayo serikali yake imetimiza katika harakati zake za kuuboresha uchumi.

#### 4.2.1.4 Kuendeleza Uwiano na Utangamano wa Kitaifa

Kulingana na Taasisi ya NCIC (2012) uwiano na utangamano wa kitaifa unahusisha umoja, usawa, uhuru, demokrasia, kutokuwa na vita, amani ya haki, haki ya kijamii na kuzingatia kanuni za sheria. Uwiano husaidia kukuza ushirikiano wa kimaadili na kuendeleza maisha. Suala hili limejitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti umebainisha kuwa kila mwanasiasa huwarai wananchi na wapigaji kura kudumisha amani na kuwaeleza kuwa lengo lao kuu ni kuwaleta Wakenya pamoja. Kwa mfano, Ruto (2021) anasema:

> Mimi ninataka niwaulize wale waliosambaratisha chama ya Jubilee, walitaka tukose mbinu na namna tutawanyike, watuingize katika siasa ya ukabila na chuki, sisi tunawaambia tumewaonea mbali na tumejipanga sawa sawa. Hata kama mmesambaratisha chama ya Jubilee, Mungu ametusaidia tuko na chama ya UDA na Wakenya wengi wamekubali chama ya UDA tuunganishe Wakenya wote kutoka sehemu zote na tutengeneze Kenya ijayo pamoja vile tulitengeneza serikali hii tuliyo nayo.

Mwanasiasa huyu anadhihirisha nia yake ya kuendeleza amani na uwiano wa kitaifa. Anasema kuwa lengo lake na chama chake ni kuwaunganisha Wakenya, kuendeleza umoja kwa kuzuia chuki na ukabila. Masuala haya yote yanadhihirisha maudhui ya kuendeleza utangamano wa kitaifa. Naye Odinga (2017) anasema kuwa yeye ameendeleza uwiano wa kitaifa kwa kuwaaunganisha Wakenya katika mikoa yote nchini ambako ana wafuasi, anasema:

> Sasa siku ya leo, nataka tu kutoa shukrani kwa Wakenya wote kutoka pembe zote za Kenya. Tumeagana na Wakenya kule Mkoa wa Magharibi, Mkoa wa Nyanza, Bonde la Ufa, Nairobi, Mkoa wa Katikati, Mashariki, Mashariki Kaskazini na Pwani na wote wamesema Raila na Kalonzo tosha.

Katika kauli hii yake, anaonyesha yeye kama kiongozi amepata uungwaji mkono katika kila eneo. Anaonyesha jinsi yeye anavyofaa kuchaguliwa kwani ameweza kuwaunganisha. Huku ni kuendeleza uwiano na utangamano wa kitaifa. Kenyatta (2022) anaendeleza haya. Anasema:

> Lakini la muhimu zaidi, mimi nina hakika ya kwamba wakati atashika usukani, hatawaacha ndugu na dada zake nyuma. Wakati serikali itaundwa utasikia Kalonzo Musyoka, tutasikia Gideon, tutasikia Charity Ngilu. Tutasikia nani, nani na nani. Hata wewe Alfred Mutua bado uko huko.

Mhes. Kenyatta anasema maneno haya baada ya kuungana na Mhes. Odinga aliyekuwa akiwania urais. Anamuunga kwa kusema yeye angeunda serikali ya muungano wa kitaifa ambayo ingejumuisha viongozi wote. Hili ni tendo la kuwaleta Wakenya pamoja, kwani viongozi hawa wana wafuasi wao. Hili linabainisha wazi kuwepo kwa maudhui ya uwiano na utangamano wa kitaifa.

### 4.2.2 Kuchimuza Fani au Tamathali za Usemi

Wamitila (2003) anasema kuwa tamathali za usemi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliypokusudiwa na mtunzi.

Clinton na Ilyin (1993) wanasema kuwa tamathali husaidia kuelewa dhana ngumu na iliyo dhahania kwa kutumia wazo linalofahamika. Wanasema kuwa hufanya mambo kadha wa kadha katika matini za kisiasa kama vile kusihi, kuonyesha umoja na kutotaja dhana fulani wazi. Utafiti huu umeonyesha jinsi wanasiasa wametumia tamathali za usemi kuhamasisha wananchi kwa kuonyesha jinsi wanavyonyanyaswa na viongozi fulani pamoja na kuwasuta viongozi hao. Tamathali ni kipengele cha

kimtindo katika kazi ya fasihi jinsi ulivyo usimulizi unaorejelewa katika nadharia ya Naratolojia. Vipengele vya usimulizi vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi vimeweza kubainisha wazi baadhi ya tamathali za usemi zitakazojadiliwa katika sehemu hii. Aidha, aina nyingi za tamathali zimetumiwa na wanasiasa katika hotuba zao, ni mbili tu ambazo zitarejelewa katika utafiti huu.

#### 4.2.2.1 Majazi

Majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika majina kulingana na sifa au tabia zao. Kamusi ya Karne ya 21 (2014) inafafanua majazi kwa kusema kuwa ni jina analopewa mtu ambalo hufanana na tabia au umbile lake. Utafiti huu umeonyesha matumizi ya majina ya majazi pale wanasiasa wanapowasuta wapinzani wao. Kwa mfano, hotuba ya Mhes. Ruto huko Nakuru tarehe 2/10/2021 katika mkutano wa kampeni yake kama mwaniaji wa kiti cha urais anasema:

> *So* Bw. Kitendawili wacha kudanganya watu ati kulikuwa na *constituency*. Wewe ulikuwa wapi *for four years* na *handshake* yako. Mbona *hamku-constitute* IEBC ndio ifanye mambo ya *constituency* kulingana na sheria *section 89* ya Katiba ya Kenya?

Katika kauli hii, Mhes. Ruto anampa mpinzani wake wa kiti cha urais jina la majazi Bw. Kitendawili. Jina hili linasawiana na tabia yake Mhes. Odinga ya kupenda kutega na kutegua vitendawili wakati wa mikutano yake ya kisiasa. Majazi yanajitokeza pia katika hotuba yake Odinga anaposimulia mechi dhahania ya kandanda kati ya timu yake ODM na ile ya Tangatanga kutoka Jubilee, anasema:

> Hii mchezo itachezwa, refarii ni Bw. Chebukati. Sasa timu ni mbili. Ile nyingine imevaa *jersey* nyekundu na ingine imevaa *jersey* ya machungwa, sawa? Nimeona timu zinaingia kwenye kiwanja. Ile timu ya Tangatanga *captain* anaitwa, anaitwa nani? Ati nani? Ati nanii? Arap Mashamba, nimeona Arap Mashamba ameingia pale ameshikwa mkono na Mariga. Ati Mariga ndio *forward* wao!

Majina Tangatanga na Arap Mashamba ni majina ya majazi. Neno Tangatanga ni jina walilopewa wanasiasa waliokuwa wanamuunga mkono Ruto kinyume na matarajio ya kinara wao katika chama cha Jubilee. Wanaitwa hivi kwa sababu walikuwa wakizunguka Kenya nzima wakitafuta kura kabla ya kipindi cha uchaguzi kufika. Aidha, Ruto anaitwa Arap Mashamba na mpinzani wake Odinga. Jina hili anabandikwa baada ya kushutumiwa katika sakata kadhaa za unyakuzi wa ardhi hasa ya umma, japo kuna baadhi ya kesi hizi zinazopuuzwa na mahakama. Badala ya Odinga kumtaja moja kwa moja kwa kusema yeye anaibia watu mashamba, anatumia jina hili. Obeng (1997) anaeleza kuwa tamathali hutumiwa ili kujiepusha kuzungumzia wazi kuhusu miiko katika jamii husika, jinsi mnenaji anajiepusha kumshutumu. Mrejelewa anapewa jina hili kutokana na tamaa yake ya mashamba.

#### 4.2.2.2 Sitiari

Kamusi ya Karne ya 21 (2014) inaeleza kuwa sitiari ni tamathali ya usemi ya kuhusisha kitu kimoja na kingine chenye sifa zinazofanana. Sitiari huhusisha uainishaji wa kisemantiki ambapo dhana moja inahusishwa na nyingine ambapo lugha ya ujanja hutumika. Utafiti huu umeonyesha jinsi wanasiasa hulinganisha dhana fulani na nyingine wanapotumia sitiari. Kwa mfano, mwaka 2017 Mhes. Odinga anapoanza kuwahutubia wafuasi wake pale katika Bustani ya Uhuru anasema:

> Hayaa! Vijana hoyee! Nairobi hoyee! Leo, wale ambao walikuwa na tashwishi watajua kuna *Tsunami*. Nilisema *tsunami* itakuja. Imeanza leo, kuelekea tarehe nane. Nane nane nane. Ni nane mara tatu.

Neno *tsunami* limetumika kiistiari. Kwa kawaida, *tsunami* ni wimbi kubwa la bahari ambalo hutetemesha sehemu za pwani. Anapolitumia katika kauli yake, anafananisha na wimbi kubwa la mabadiliko ambalo lingesababishwa naye baada ya kuchaguliwa

siku ya uchaguzi ambao ungefanyika tarehe nane. Steinhart na Kitany (1998) wanasema kuwa sitiari husaidia kutega usikivu wa umma. Hili linadhihirika wazi Odinga anapotumia kauli hii mwanzo mwanzo wa hotuba yake. Odinga anaendelea kudhihirisha sitiari anaposema:

> Sisi tumesema kama wana-NASA tukishika, tutavuka, siku ya Jumanne, alfajiri ni sisi tuvuke Mto Jordan, tutoke Mto Jordan tuingie pande ile nyingine ya Canaan, sindio? Saa kumi na mbili tutaanza safari sio?

Katika kauli hii, Odinga anarejelea Mto Jordan na Canaan. Kiistiari anadhihirisha kuwa mpaka kati ya Wakenya na yale maendeleo ambayo angewaletea kama rais ni sawa na Mto Jordan. Nayo maendeleo ambayo angewaletea na kulitendea taifa ni sawa na Canaan ile iliyoko katika Biblia iliyosemekana kuwa nchi iliyojaa maziwa na asali kulingana na Kutoka 3:8 (NKJV) Msimulizi anajilinganisha na Joshua wa Biblia aliyewasaidia Wanaisraeli kuingia Canaan. Haya ni matumizi ya sitiari kwani ushindi wake ungekuwa sawa na Wakenya kuingia "Canaan" katika maendeleo ambayo angeyafanya. Fani hii imejitokeza katika hotuba ya Ruto (2021) pia, anasema:

> Mtatupatia gavana wa UDA ambaye atasukuma *project* ya *Bottom Up*, na seneta tuko pamoja? Mtatupatia hawa wote tutembee pamoja? Na mtachagua rais ambaye anajua *Hustler Nation* ni nini Kenya? Tuko pamoja jameni?

Katika kauli hii, anatumia jina *Hustler Nation*, neno hili limetumika kiistiari kuwarejelea Wakenya ambao wanahangaika na hali ngumu ya kiuchumi lakini hawafi moyo bali wanaendelea kujibidiisha ili kufaulu maishani. Anasema kuwa rais atakayechaguliwa anafaa kuwa yule anayewaelewa na amepitia hali kama hio ya maisha. Anatumia vuguvugu hili kuwavutia na kuwahamasisha wafuasi wake. Leech

(1969) anaeleza kuwa tamathali husaidia kuhamasisha zaidi kuhusu jambo fulani kwa mfano anawajuza wafuasi na kuwakejeli wapinzani wake Odinga na Kenyatta waliozaliwa katika familia za kitajiri na hawaelewi hali ya kukosa na kukazana ili kufaulu maishani.

### 4.3 Hitimisho

Sehemu hii ilishughulikia kipengele cha uwasilishaji usemi pamoja na dhima za wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi. Ilibainisha kuwa usemi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya huwasilishwa katika usemi halisi, usemi taarifa na usemi halisi huru isipokuwa usemi taarifa huru ambao haukujitokeza. Aidha, imeonyesha kuwa dhima kuu za vipengele: wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi katika hotuba teule za wanasiasa ni kuchimuza maudhui na fani au tamathali za lugha.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulihusu wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti ulielekezwa kwa kutumia nadharia ya Naratolojia. Dhamira ya utafiti huu ilikuwa ni kubainisha jinsi vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika vinavyojitokeza pamoja na dhima zake katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Sura hii inahusu muhtasari wa utafiti na matokeo ya utafiti yanayofafanua iwapo malengo ya utafiti yalitimizwa au la. Umuhimu wa utafiti huu umejadiliwa hapa pamoja na matatizo yaliyoukumba utafiti huu. Itatoa mapendekezo kuhusu tafiti zitakazofanywa kuhusu hotuba yoyote ile na suala la usimulizi kuhusu hotuba na usimulizi kwa ujumla.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuonyesha jinsi vipengele vya usimulizi vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika vinavyojitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Halikadhalika, utafiti ulilenga kuonyesha dhima ya vipengele hivi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Hotuba zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti ni zile kauli ambazo wanasiasa huzitoa wao wenyewe katika mikutano ya kisiasa bali si hotuba rasmi ambazo wao huzitoa kwa kuzisoma. Hii ni kwa sababu huenda baadhi ya hotuba rasmi, huwa wameandikiwa, jambo ambalo lingeupa utafiti upungufu kwani utafiti uliwalenga watafitiwa wenyewe binafsi. Wanasiasa waliorejelewa ni Mhesh. Raila Odinga, Mhesh. Uhuru Kenyatta na Mhesh. William Ruto. Utafiti uliteua hotuba tatu zilizotolewa na kila mwanasiasa katika mikutano ya kisiasa kati ya mwaka 2013 hadi 2022 ambapo ilibainika wazi kuwa hotuba hizi

zimefumbata kwa kiasi kikubwa vipengele rejelewa vya usimulizi vilivyochunguzwa katika utafiti huu. Nadharia iliyorejelewa kuelekeza utafiti huu ilikuwa nadharia ya Naratolojia, vipengele vyake ndivyo vilivyotumika kama mihimili. Vipengele hivi vilikuwa wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi. Mtafiti alizingatia mawazo yake Mwananaratolojia Rimmon-Kenan katika kuufanya utafiti huu.

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza imefafanua istilahi zilizotumika, usuli wa tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti. Aidha, sura ya kwanza ina maelezo kuhusu nadharia iliyotumika, mbinu za utafiti na usampulishaji pamoja na maelezo mafupi kuhusiana na baadhi ya tafiti zinazohusiana na utafiti huu.

Kuna sura ya pili ambayo imeshughulikia lengo la kwanza la utafiti huu: kubainisha kipengele cha wakaa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Sura hii imebainisha vipengele vya wakaa na jinsi vinavyojitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Vipengele hivi ni mpangilio ambapo analepsia na prolepsia yamejadiliwa kwa mapana, kipengele cha muda ambapo udondoshi, mtuo, muhtasari na onyesho yamejadiliwa na umara au idadi marudio.

Sura ya tatu imeshughulikia lengo la pili ambalo limebainisha kipengele cha wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti umeonyesha jinsi wanasiasa wanavyowasawiri wanasiasa wenzao katika hotuba zao. Sura ya nne nayo imeshughulikia malengo mawili. Imebainisha uwasilishaji usemi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya kwa kuonyesha mbinu za uwasilishaji usemi za usemi halisi, usemi taarifa, usemi halisi huru na usemi taarifa huru pamoja na kuonyesha dhima za

vipengele vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu uliohusu wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya uliongozwa na madhumuni manne. Usimulizi huhusishwa na tungo za kinathari, utafiti huu umebainisha kuwa hotuba ni mojawapo wa tungo za kinathari. Utafiti umedhihirisha haya kwani umebainisha kuwa vipengele vya usimulizi vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi vimetumika katika hotuba teule zilizorejelewa. Aidha utafiti umeonyesha kuwa vipengele hivi vina dhima kubwa katika kuwasilisha ujumbe wa hotuba.

Katika sura ya pili ambapo lengo la kwanza la utafiti limeshughulikiwa, kipengele cha wakaa kimerejelewa, utafiti huu ulibaini kuwepo vipengee vya mpangilio, muda na idadi marudio katika hotuba teule. Utafiti umeonyesha jinsi matukio yalisimuliwa kwa kuzingatia anakroni katika kipengee cha mpangilio. Aina za anakroni kama vile analepsia zimejitokeza katika hotuba za wanasiasa Odinga, Ruto na Kenyatta. Aina za analepsia zilizojitokeza ni kama vile analepsia tawasifu, analepsia wasifu, analepsia ya nje, analepsia ya ndani na analepsia mseto zimejitokeza. Aina nyingine ya anakroni ya prolepsia imejitokeza. Aina za prolepsia ambazo ni prolepsia tawasifu, prolepsia wasifu, prolepsia ya nje, prolepsia ya ndani na prolepsia ya mseto zimejitokeza. Utafiti pia umebainisha vipengee vya muda vya udondoshi bayana, udondoshi usio wazi, udondoshi batini na udondoshi dhahiri vimejitokeza japo udondoshi dhahiri ulijitokeza kwa uchache katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Utafiti pia umebainisha wazi kuwa katika kipengee cha idadi marudio usimulizi rudufu ulijitokeza. Utafiti umeonyesha kuwa usimulizi mosi haujajitokeza katika hotuba

teule za wanasiasa wa Kenya. Hii ni kwa sababu wanasiasa wanamazoea ya kujirudiarudia kauli katika mikutano ya kisiasa ili kusisitiza ujumbe na kwa kuwa kile wanachopigania huwa katika manifesto au ruwaza zao wanazotumia ili kuungwa mkono na kuwaelekeza katika uongozi wao endapo watangeibuka washindi katika uchaguzi.

Lengo la kubainisha uwasilishaji usemi na dhima za wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi lilishughulikiwa kwa kuonyesha kuwa wanasiasa teule walitumia kipengele cha uwasilishaji usemi kama mbinu mojawapo ya kueleza ujumbe katika hotuba zao. Hili limerejelewa katika sura ya nne. Baadhi ya mbinu za uwasilishaji usemi zilizotumiwa na kujitokeza katika hotuba teule za wanasiasa ni kama usemi halisi, usemi taarifa na usemi halisi huru. Utafiti huu ulionyesha kuwa mbinu ya usemi taarifa huru haijatumiwa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya. Aidha, utafiti umebainisha wazi kuwa hotuba ikiwemo hotuba za wanasiasa teule wa Kenya hutumia kwa wingi mbinu ya uwasilishaji usemi ya usemi halisi. Hii ni kwa kuwa kauli zao hutolewa moja kwa moja na wao binafsi wanapowahutubia wafuasi wao katika mikutano ya kisiasa. Hii imeonyeshwa wazi katika data iliyorejelewa na utafiti huu.

Katika lengo la kubainisha jinsi wahusika wanavyosawiriwa katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya, utafiti huu umeonyesha kuwa wanasiasa teule waliweza kuwasawiri wahusika katika simulizi zao kupitia mbinu za usawiri wa moja kwa moja ambapo wanasiasa walitumia kauli za wazi zilizodokeza sifa za wanasiasa wenzao ambao waliwarejelea kama wahusika katika simulizi yao. Usawiri usio wa moja kwa moja ulibainishwa na kuonyeshwa jinsi unavyojitokeza, hapa wahusika walisawiriwa kwa kurejelea usemi wao, matendo na mazingira yao. Utafiti ulionyesha kuwa wahusika hawakusawiriwa kupitia muonekano wa nje kwani hakuna mwanasiasa

aliyetoa kauli yoyote kuhusiana na maumbile ya mwenzake ili kutoa sifa zake. Japo data lerejelewa ilikuwa video za *YouTube* zilizonyesha muonekano wao wahusika, mtafiti alilenga tu kile walichosema bali sio kile alichokiona.

Mwishowe, utafiti huu uliweza kubainisha kuwa dhima za vipengele vya wakaa, wahusika na uwasilishaji usemi katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya ni kuchimuza maudhui, baadhi ya maudhui yaliyojitokeza katika hotuba hizi ni ufisadi, utangamano wa kitaifa, siasa na Uchumi. Dhima yavyo nyingine iliyojitokeza ni kuwa vipengele hivi vimetumika kuchimuza fani au tamathali za usemi. Baadhi ya tamathali za usemi zilizojitokeza katika hotuba teule za wanasiasa wa Kenya ni majazi na istiari.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wasomi na watafiti wa Fasihi ya Kiswahili kwa kuwajuvya kuhusu uchanganuzi wa mtindo wa usimulizi katika hotuba. Aidha, mapengo yaliyowachwa wazi na tafiti zilizotangulia kuhusu hotuba nyingi zilizokuwepo zikishughulikia masuala mengine ya kimtindo ambayo hayakuhusiana na mtindo wa usimulizi yamezibwa.

Kwa kulizamia suala la usimulizi katika nadharia ya Naratolojia, utafiti huu utawafaa wasomi kwa kuwapa marejeleo ya kupitia ili kuelewa suala hili kwa undani.

## 5.4 Matatizo yaliyoukabili Utafiti

Ingawa utafiti huu uliweza kutimiza malengo yake matatu, kulikuwa na baadhi ya changamoto zilizoukumba utafiti huu. Mosi lilikuwa jambo la uchache wa tafiti nyingine zilizofanywa kwa kurejelea nadharia ya Naratolojia kwa kurejelea mawazo yake Rimmon – Kenan yaliyo katika lugha ya Kiingereza.

Tatizo jingine lililojitokeza ni uhaba wa vitabu, makala na majarida ambayo yameandikwa katika lugha ya Kiswahili hasa kuhusiana na nadharia ya Naratolojia. Mtafiti hakuwa na budi kusakura mtandaoni na kutafsiri makala na vitabu hivi vilivyoandikwa katika lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili hivyo kuchukua muda ambao haukuwa umepangiwa na wakati mwingine tafsiri kujitokeza kuleta maana ambayo haikuwa imekusudiwa, japo kwa kumakinika alipata maana lengwa.

### 5.5 Mapendekezo

Suala la usimulizi ni suala pana, utafiti huu ulirejelea vipengele vitatu pekee vya usimulizi vya wakaa, uwasilishaji usemi na wahusika. Kuna vipengele vingine vya usimulizi ambavyo havijarejelewa. Utafiti huu unapendekeza vipengele hivyo vingine kama vile mtazamo na daraja ya sauti vifanyiwe utafiti kwa kurejelea hotuba za wanasiasa, aina nyingine za hotuba na vipera vingine vya fasihi simulizi ambavyo ni vya kinathari.

Utafiti unapendekeza pia, tafiti zifanywe kuhusu usimulizi kwa kuzingatia hotuba rasmi kwani utafiti huu ulijikita tu kwenye hotuba zisizo rasmi. Data ya matandao wa *YouTube* iliyorejelewa ilihusu tu kauli za wanasiasa za moja kwa moja ambazo walitoa katika mikutano yao ya kisiasa.

Tafiti nyinginezo zinaweza kufanywa kwa kuzingatia nadharia ya Naratolojia hususan kwa kuzingatia mawazo yake Rimmon-Kenan ambayo yamerejelewa katika utafiti huu. Aidha, utafiti zaidi unapendekezwa kufanywa kuhusu dhima za vipengele vya usimulizi. Hii ni kwa sababu ni dhima chache zilizobainishwa na utafiti huu ili kupunguza kujirudia.

## 5.6 Hitimisho

Sura hii imetoa muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti yameelezwa huku uhakiki wa kina kuyahusu ukitolewa, mchango wa utafiti ukabainishwa, matatizo yaliyoukabili utafiti yamedokezwa na mbinu ya kukabili baadhi yavyo kufafanuliwa na mapendekezo ya tafiti za baadaye kuhusu hotuba kwa ujumla, hotuba za kisiasa na suala la usimulizi katika hotuba kutolewa.

## MAREJELEO


Adero, M. (2005). Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya kuanzia Mwaka 2002 hadi 2005. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Arege, T. (2012). Narration in Swahili Narrative Poetry: An analysis of *Utenzi wa RASI 'L GHULI*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Aristotle (1920*). The Poetics*. Oxford: Clarenton press.

Ashcroft, B., Griffiths, G., & Tiffin, H. (2013). *The empire writes back: Theory and practice in post-colonial literatures* (2nd ed.). Routledge.

Asige, N. (2021) Uchanganuzi wa Usimulizi kama Mtindo katika *Nyimbo za Bahati Bukuku*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Aswani, B., Mayaka, G. na Matinde, R. (2013). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers, Tanzania.

BAKIZA (2010). *Kamusi ya Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Bal, M. (2009) Naratolojia: *Introduction to the Theory of Narrative*. Toronto: University of Toronto Press.

Barry, P. (1995). *Beginning Theory*. New York: Manchester University Press.

Barthes, R. (1970) *An Introduction to the Structural Analysis of Narration Discourse*. Blackwell: Oxford University Press.

Chatman, S. (1978). *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca, New York: Comell University Press.

Chomsky, N. na Herman, E., (1988) Manufacturing Consent: *The Political Economy of the Mass Media*. Pantheon Book Publishers.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse*: New York: Cornel University Press.

Griffith, K. (2010). *Writing Essays About Literature*. Cengage. Wadsworth Publishers.

Habwe, H.J. (1999) *Discourse Analysis of Swahili Political Speeches*. PHD Thesis, University of Nairobi.

Keen, S. (2003). *Narrative Form*. London: Macmillan.

Keltner, D., Gruenfeld, H. na Anderson, C. (2003) Power, Approach, and Inhibition. Psychological Review.

Kinga, J.A. (2020). Matumizi ya Wakaa katika Usimulizi wa Riwaya ya Kiswahili: Mfano kutoka *Nagona* na *Mzingile*. Tasnifu ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dodoma.

King'ei, K. na Kisovi, C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Khamis, B.S. (2015). Uhakiki wa Usimulizi katika Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kothari, R. (1985) *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Easton Limited.

Kothari, R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*, (second edition). New Delhi: New Age International Publishers.

Kwaka, A. (2018) Uhakiki wa wakati na uwasilishaji usemi katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Landa, J.A. (1990). *Narrative Theory*. University of Zaragoza.

Lwaitama, F. (1988) Hotuba za Kisiasa katika Kiswahili: *Mtindo wa Maongezi ya Wanasiasa wa Tanzania (Nyerere na Mwinyi)* Dar es Salaam; University of Dar es Salaam.

Lwaitama, A.F. (1995). *A Critical Language Study of Tanzania Kiswahili Presidential Political Oratory*. PhD Thesis. Birmingham Department of Modern Languages. Birmingham: Aston University.

Mdee, N.W. (2014). *Kamusi ya Karne ya 21.* Longhorn Publishers.

Miller, D. (1995) *On Nationality*. Clarendon Press. ISBN: 97801198280477.

Mohammed, O., (2020). Election Violence in Kenya: *A Case Study of Nakuru 1992 - 2008*. Thesis for Masters digree. Kenyatta University.

Msanjila, P. (1989) *Sociolinguistic Rules of Formal Address in Kiswahili* in D.P.B Massamba et al (ed) Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili vol. 56; Dar es Salaam; TUKI.

Muiya, P. (2022) Muundo wa Usimulizi wa Riwaya ya Kiswahili: *Uchanganuzi wa Vuta N'Kuvute*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mulama, S.J. (2011). Usimulizi katika *Utenzi wa Siri Li Airali*. University of Nairobi.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Musa, Y.S. (2015). Uchanganuzi wa Hotuba za Mwalimu Nyerere kwa Mkabala wa *Nadharia ya Balagha*. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Egerton.

NCIC (2012) *Uwiano na Utangamano wa Kitaifa* – Mwongozo wa Mafunzo. Wizara ya Haki, Uwiano wa Kitaifa na Maswala ya kikatiba.

Ngowe, E., (2017). Elimu Mtandaoni. 254 blogspot

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Obeng, S.G. na Hatford, B. (2002). *Surviving Through Obliqueness; Language of Politics in Emerging Democracies. New York*. Nova Science Publishers, Inc.

Obondo, F., Okello, D., & Nandwa, R., (2017). *Mwongozo wa Kigogo*, Nairobi: StoryMoja Publishers

Oluchili, W. (2024) Usawiri wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia teule za *Kinjekitile, Jogoo Kijijini na Arusi.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Ong'ondi, B. (2005). Uhakiki wa Usimulizi katika Riwaya ya *Walenisi*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Plato. (1930). *The Republic, Books 1 to 5 trans. P. Shorey.* Cambrigde: Havard University Press.

Ponera, A. S (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dar esalam: Karljamer Print Technology.

Prince, G. (1973). *A grammar of Stories: An Introduction*. The Hague – Paris. Walter De Gruyter.

Propp, V. (1968). *The Morphology of the Folk Tale*. The American Folk Society and Indiana University Press. Texas.

Raglan, L. (1956). *The Hero: A study in Tradition Myth and Drama*. New York: Vintage Books.

Rimmon-Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction*. London: Methuen& Co. Ltd.

Rimmon-Kenan, S. (2002). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge.

Rose-Ackerman, S. (2016). *Corruption and government: Causes, consequences, and reform*. Cambridge University Press.

Senkoro, E.M.K. (2011). *Fasihi.* Dar esalam: KAUTTU Ltd.

Simiyu, W. (2015). *Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika*, Embalu na Mwaka kongwa. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Smith, J. (2021). *The psychology of betrayal: Understanding trust and loyalty in relationships*. Academic Press.

Stanzel, F. (1984). *A theory of Narrative*. London: Cambridge University Press.

The Holy Bible: (1982) *New King James Version*. Thomas Nelson

TUKI, (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi, Focus Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Publishers

Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

**Kiambatisho A: Tovuti za hotuba**

www.citizen.digital/news/the-six-pillars-of-dp-rutos-bottom-up-economic-model

www.elections.nation.africa

www.iebc.co.ke/election/?election-results

www.ipsos.com/en/kenya-2017-poll-two-horse-race

www.youtube.com/watch/v=rTU3akPgErU

www.youtube.com/watch?app=desktop&v=284Ch224rxQ

www.youtube.com/watch?v=4UfEtaBiaA4

www.youtube.com/watch?v=dR440W_n4XQ

www.youtube.com/watch?v=InGgRa2ZrEo

www.youtube.com/watch?v=KvXdWzOZq0M

www.youtube.com/watch?v=ONd8ye-wfb4&t=479s

www.youtube.com/watch?v=QR6TvEiGmWg

## Kiambatisho B: Kibali cha utafiti

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **557646**

Date of Issue: **27/February/2025**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. Stanley Kekonen Mukonambi of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nairobi on the topic: WAKAA, UWASILISHAJI USEMI NA WAHUSIKA KATIKA HOTUBA TEULE ZA WANASIASA WA KENYA for the period ending : 27/February/2026.**

License No: **NACOSTI/P/25/416475**

**557646**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation,** hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to.
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. Neither the license nor any rights thereunder are transferable.
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke